# Nipashe

Alhamisi Februari 15, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581587

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**PUTO MUHIMBILI** Apungua kilo 55 siku 385



UKURASA 4

**MAHAKAMA** yatoa amri nyumba ya mtoto wa Mbowe ipigwe mnada

UKURASA 5

**TANZANIA** yaandika historia mkutano wa Samia na Papa Francis Vatican

UKURASA 8




UKURASA 11

KIFO CHA LOWASSA

# Minong'ono jeneza lake kutofunguliwa

**ASKOFU** Malasusa avunja ukimya, viongozi wasioshiriki ibada wapewa angalizo; Katibu Mkuu CCM... *Endelea ukurasa 2 & 3*



Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, akiongoza ibada ya kuombea mwili wa Waziri Mkuu mstaafu, Hayati Edward Lowassa, katika Kanisa la Azania Front jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Slaa, Mwabukusi wajitosa kushiriki maandamano ya CHADEMA leo

UKURASA 4

## Deni la Serikali laongezeka kwa trilioni 12.72/- mwaka mmoja

UKURASA 3

## Rais Samia: Ukuaji uchumi kupandisha chati Tanzania 2024

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akiwasili katika Kasri la Kifalme pamoja na Mwenyeji wake, Mfalme Harald V wa Norway kwa ajili ya kushiriki dhifa ya kitaifa jijini Oslo juzi. **PICHA: IKULU**

**MICHEZO** YANGA YAVUNJA REKODI LIGI KUU UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Mjane wa Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, Regina Lowassa, akilia kwa uchungu, wakati wa ibada ya kumuaga mume wake katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Usharika wa Azania Front jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Malasusa avunja ukimya kuhusu jeneza la Lowassa kutofunguliwa

**Na Jenifer Gilla**

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa, amevunja ukimya kuhusu maswali yaliyokuwa yakihoji watu kutokutazama mwili wa aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa, wakati wa kuaga.

Tangu kuanza kutolewa kwa heshima za mwisho juzi, kumekuwa na maswali mengi yaliyokosa majibu kwa nini jeneza lenye mwili wa kiongozi huyo halikufunguliwa ili watu kuona kama ilivyo desturi katika kuaga miili ya marehemu kwa waumini wa madhehebu ya Kikristo.

Kutokana na utata huo, Askofu Dk. Malasusa alisema si lazima jeneza kufunguliwa bali inatokana na utashi wa wahusika.

"Hakuna ulazima katika kanisa kuufungua au kuona mwili wa mwanadamu aliyefariki dunia," alisema Dk. Malasusa wakati wa ibada ya kuaga mwili wa Lowassa katika ibada iliyofanyika jana katika Kanisa Kuu la KKKT Usharika wa Azania Front.

Lowassa alifariki dunia Jumamosi iliyopita katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dar es Salaam, alikokuwa akipatiwa matibabu na anatarajiwa kuzikwa nyumbani kwao, Monduli mkoani Arusha.

Aidha, Dk. Malasusa ambaye ni Askofu wa KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani, aliwakumbusha viongozi wa serikali kufanya ibada ili wanapofariki dunia wapelekwe kanisani kufanyiwa ibada.

Pia aliwasisitiza wasiwalazimishe viongozi wa dini kupelekwa kanisani kwa ajili ya kufanyiwa ibada wanapokutwa na umauti kwa sababu ya vyeo vyao wakati hawashiriki ibada wangali hai.

Wakati Dk. Malasusa akisisitiza hayo, Mchungaji Kiongozi wa KKKT Usharika wa Kijitonyama, Dk. Eliona Kimaro, amesema Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, atakumbukwa Tanzania na Afrika kwa mchango wake katika maendeleo ya elimu.

Malasusa aliwasihi wachungaji wa KKKT kutoingiza mwili wa marehemu kanisani kwa ajili ya kufanyiwa ibada ilhali wakati wa uhai wake hakupenda kushiriki ibada huku akieleza kufurahishwa kuona watu mbalimbali walivyokuwa wakimshuhudia Lowassa kuwa alikuwa mpenda ibada.

Kwa mfano wa Lowassa, Askofu Dk. Malasusa aliwasihi viongozi kujenga tabia ya kumwabudu Mungu wakiwa hai ili kumshukuru kwa kuwapa watu wa kuwaongoza na awape rehema ya kuendelea kuwatumikia.

"Kiongozi wa watu anayependa ibada anamjua Mungu aliyempa watu wa kuwaongoza na anamsikiliza ili ampe uwezo wa kuwaongoza," alisema.

Askofu Malasusa alitoa pole kwa familia ya Lowassa kwa msiba huo mkubwa uliogusa maisha ya watu na kuwasihi kumtegemea Mwenyezi Mungu katika kipindi hiki kwa kuwa kila jambo linalotokea kwa wakati wake.

"Kuna wakati wa kuzaliwa. Edward Lowassa alizaliwa na kuna wakati wa kufa, kuna wakati wa kulia na wakati wa kucheka," alisema Askofu Malasusa.

**MCHUNGAJI KIMARO**

Naye Mchungaji Dk. Kimaro alisema kiongozi huyo (Lowassa) atakumbukwa Afrika kwa mchango wake mkubwa wa kuboresha elimu ili kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anapata elimu ya sekondari.

Alisema wakati yeye (Kimaro) anasoma, wanafunzi wengi walikuwa wanafaulu lakini walichaguliwa wachache kutokana na uhaba wa shule tofauti na sasa ambapo mwanafunzi akimaliza darasa la saba, anakwenda sekondari moja kwa moja.

**KAULI ZA WANASIASA**

Aliyewahi kuwa Mbunge wa Busega (CCM), Dk. Raphael Chegeni, alisema kanisani hapo kuwa anaamini mwanasiasa huyo angeendelea kuishi zaidi kama isingekuwa ajali mbalimbali za kisiasa alikumbana nazo.

Chegeni alisema siasa zilimletea kiongozi huyo migogoro lakini alisimama kama kiongozi na kuacha alama akiongozwa na upendo.

"Hata alipopata ajali ya kisiasa, aliamua kujiuzulu ili kulinda heshima yake jambo ambalo viongozi wachache sana wanaweza kulifanya," alisema.

Mwanasiasa huyo aliyekuwa mfuasi wa Lowassa katika harakati za kisiasa, alisema alikutana naye Lowassa bungeni mwaka 2001 akiwa Waziri wa Maji na Mifugo na alifanya mambo makubwa hasa alipoteuliwa kuwa Waziri Mkuu mwaka 2006.

Chegeni alisema mwaka 2015 walianza safari ya matumaini na popote walipokwenda na Lowassa, Watanzania waliwapa msaada mkubwa kwa inami waliokuwa nayo kwake kuwa anaweza kuwaletea maendeleo.

Alisema ametoka Mwanza kushiriki mazishi ya kiongozi huyo kwa mapenzi aliyo nayo na yale mema aliyoyatenda.

Naye Naibu Waziri wa zamani wa Viwanda na Biashara; na Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ritha Mlaki, alisema kwa miaka 48 aliyomfahamu Lowassa, alikuwa muwazi na hakuweka vitu rohoni.

"Alikuwa mchapakazi mahiri, mwenye sauti iliyojaa mamlaka, alipenda haki na katika kipindi cha Kwaresma alifunga siku zote 40," alisema.

Mlaki alisema Lowassa alimfundisha kumtaja Mungu kila anapoanza kutoa hotuba na kuzungumza kwa sauti kubwa, kupenda na kuwajua watu wengi iwezekavyo.

"Mtu akikusalimia hata kama humjui we mjibu tu. Akikuuliza unanikumbuka mwambie ndiyo halafu muulize hivi nilikuona wapi wewe. Hivi ndivyo alivyonifundisha Lowassa," alisema Mlaki.

Pia alisema alimfundisha kuwa mwangalifu na maneno anayoyazungumza hadharani kwa sababu akikosea hataweza kuyarudisha mdomoni.

Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ruth Mollel, alisema Lowassa alimshawishi kuingia kwenye siasa tangu wakiwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Alisema amejifunza mambo mengi kutoka kwa kiongozi huyo ikiwamo ujasiri na uthubutu kwani akiwa na lengo lake atasimama hadi litimie.

Mollel alisema Lowassa alikuwa na hekima ya ukimya akiamini kuwa wakati mwingine ukimya ni jibu.

**PROFESA PALLANGYO**

Rafiki wa karibu wa Lowassa, Prof. Kisali Pallangyo, alisema kiongozi huyo alipenda watu na watu walimpenda na wakati anaugua, watu wengi kutoka sehemu mbalimbali walikwenda kumjulia hali.

Alisema uongozi wake (Lowassa) ulianza kuonekana alipokuwa bendi ya shule kiongozi wa brasbend wakati anasoma Shule ya Msingi Monduli (sasa Shule ya Msingi Moringe).

Prof. Pallangyo aliishukuru serikali pamoja na madaktari kwa kumhudumia Lowassa tangu alipoanza kuugua na hata kumzika kwa heshima.

# Bodaboda wamlilia Lowassa

**Na Halfani Chusi**

MADEREVA wa pikipiki za abiria, maarufu bodaboda, wameonyesha kuguswa kufuatia kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu, Hayati Edward Lowassa aliyefariki wiki iliyopita jijini Dar es Salaam.

Bodaboda hao wamelieleza gazeti hili kwamba kiongozi huyo aligusa makundi mengi likiwamo kundi lao kwa namna tofauti.

Mmoja wa madereva hao, Mengi Mfinanga, alisema mwanasiasa huyo alikuwa mpenda haki, amani na kwamba alikuwa na sera nzuri wakati alipohamia upinzani ambazo kwa kiasi kikubwa, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Magufuli, alizifanyia kazi, ikiwamo elimu bure.

"Lowassa alikuwa mtu poa sana. Ametufunza kuwa na uthubutu lakini uvumilivu. Tumeliona hilo kipindi cha uchaguzi alipopigwa chini licha ya kwamba ilionekana kama ameshinda lakini hakuwa chanzo cha vurugu.

"Alihamasisha amani na hakutaka kuona mtu anamwaga damu kwa ajili yake. Alikuwa anachukizwa na viongozi kutotimiza wajibu wao vizuri. Lowassa ni kiongozi mfano wa kuigwa," alisema.

Jakobo Ndala, dereva mwingine, alisema kiongzoi huyo alileta mageuzi makubwa ya kisiasa na ndiye kiongozi wa kwanza kutoka upinzani kupata kura nyingi zaidi katika ngazi ya urais na kwamba kilichobaki sasa ni kumwombea kwa Mungu ailaze roho yake mahali pema.

Naye Nassib Posy alisema huu ni wakati wa kuendeleza yale aliyokuwa anayaota mwanasiasa huyo, huku akisisitiza kuwa mtu hawezi kuwataja wanasiasa mahiri jina lake likakosekana.

"Alijiuzulu ili kulinda heshima yake na heshima ya chama chake. Maana yake aliweka maslahi ya taifa mbele. Kitendo kile sisi bodaboda kilitufunza kutokuwa waoga katika kufanya uamuzi na kusimamia kile tunachokiamini.

Lowassa aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania chini ya Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, kutoka mwaka 2006 mpaka 2008 alipojiuzulu kutokana na kashfa ya Richmond.

Mwaka 2015, Lowassa alijiengua Chama Cha Mapinduzi (CCM) baada ya kukatwa ngazi ya Kamati Kuu katika kinyang'anyiro cha urais kupitia chama hicho na kuhamia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na kuteuliwa kugombea urais chini ya Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) ambao mbali na CHADEMA, uliundwa na Chama Cha Wananchi (CUF), NCCR- Mageuzi na National League for Democracy (NLD). Hata hivyo, alishindwa katika uchaguzi huo dhidi ya Magufuli.

HABARI KITAIFA

# Deni la Serikali laongezeka kwa trilioni 12.72/- mwaka mmoja

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

DENI la Serikali limeongezeka hadi Sh. trilioni 87.47 Desemba 2023 kutoka Sh. trilioni 74.75 Desemba 2022, sawa na ongezeko la Sh. trilioni 12.72 (asilimia 17) ndani ya mwaka mmoja.

Kati ya kiasi hicho, Deni la Nje ni Sh. trilioni 56.79 na Deni la Ndani ni Sh. trilioni 30.67.

Jana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Daniel Sillo, alibainisha hayo wakati anawasilisha bungeni taarifa ya mwaka kuhusu utekelezaji majukumu ya kamati katika kipindi cha Februari 2023 hadi Januari 2024.

Pamoja na tathmini ya utekelezaji bajeti ya serikali kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai hadi Desemba 2023), alisema ongezeko la deni limetokana na ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi ya kimkakati.

Alisema miradi hiyo ni ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, elimu, afya, kilimo, mifugo, nishati na maji.

Mwenyekiti huyo alisema katika kipindi cha miezi sita kuanzia Julai hadi Desemba 2023, Deni la Serikali limeongezeka kwa Sh. trilioni 7.14 kutoka Sh. trilioni 80.33 mwezi Juni 2023 hadi kufikia Sh. trilioni 87.47 mwezi Desemba, 2023.

Kwa mujibu wa Sillo, uchambuzi wa kamati hiyo umebaini Deni la Nje limeongezeka kutokana na mabadiliko ya viwango vya kubadilisha fedha pamoja na riba kwa mikopo inayotegemea mabadiliko ya hali ya soko.

Alibainisha kuwa asilimia 28.3 ya Deni la Nje ipo kwenye riba inayobadilika kulingana na soko na asilimia 71.7 ya deni ina riba isiyobadilika.

Hivyo, kamati yake inashauri serikali kuimarisha makusanyo ya ndani na kuendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF) ili kuondokana na mikopo ya kibiashara, ambayo ina riba kubwa na inayobadilika kulingana na hali ya soko.

Pili serikali ihakikishe taasisi zake zinazojiendesha kibiashara zinalipa mikopo yake ili kuepuka kihatarishi cha mikopo. Mikopo ya kibiashara ielekezwe katika miradi ambayo inaleta matokeo kwa muda mfupi.



Jeneza lenye mwili wa Waziri Mkuu mstaafu, Hayati Edward Lowassa, likiwa kwenye gari maalum la Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), likiondoka katika Usharika wa Azania Front jijini Dar es Salaam jana baada ya ibada. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Nchimbi: Lowassa alikuwa jasiri, mkweli

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amesema Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, alikuwa kiongozi jasiri, mkweli, mpenda maendeleo na muumini wa kweli wa muungano na umoja wa Watanzania.

Amesema Lowassa alikuwa rafiki, kaka, mwalimu wake na mtu mwenye mchango mkubwa katika safari yake ya uongozi.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Dk. Nchimbi aliandika: "Good morning'. Hivi ndivyo alivyotusalimu Waziri Mkuu Mstaafu, Edward Lowassa, kila alipoingia kwenye kikao chochote cha kikazi, iwe asubuhi, mchana au usiku alimradi ni kazi. Salamu yake ilikuwa 'Good morning', alimaanisha kazi inaanza wekeni kila kitu pembeni tufanye kazi".

Pia aliandika: "Aliheshimu watu wote (Lowassa) bila kujali rika, nafasi au uwezo wa kifedha, akiwa rafiki yako ni rafiki yako kweli kweli. Lowassa alikuwa kaka yangu, rafiki yangu, mwalimu wangu na mtu mwenye mchango mkubwa katika safari ya uongozi."

Balozi Nchimbi alisema namna pekee ya Watanzania kumuenzi Lowassa ni kuchapa kazi kwa bidii.

"Namna pekee kwa Watanzania kumuenzi Lowassa ni kwa kuchapa kazi kwa bidii kwa sababu alikuwa mtu hodari kwa kutetea maslahi ya watu bila kujali wanakotoka, imani zao wala mlengo wao wa kisiasa. Tutamkumbuka kwa mchango wake katika ujenzi wa taifa letu," alisema Dk. Nchimbi.

Wakati huo huo, Balozi wa Tanzania nchini Ethiopia, Innocent Shio, alimtaja Lowassa kama kiongozi aliyeweka alama katika sekta ya elimu na maji na kutaka Watanzania kuyaenzi yale yote aliyoyafanya kwa taifa.

"Kikubwa kama Watanzania tuendelee kuyaenzi na kuyaheshimisha yale yote aliyoyafanya kwenye taifa letu ili tusonge mbele katika zote alizozitendea haki katika kipindi chote cha uongozi wake," alisema Balozi Shio.

# Samia: Ukuaji uchumi 2024 utaipandisha chati Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) mwaka huu, Tanzania inatarajiwa kuwa kati ya nchi 20 zenye uchumi unaokua kwa kasi duniani.

Taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus jana, Rais Samia amesema kuwa hiyo ni fursa kwa wawekezaji wa Norway kuja Tanzania kwa kuwa nchi pia ina mazingira mazuri ya kisiasa, kijiografia na kiuchumi.

Akihutubia Mkutano wa Jukwaa la Biashara kati ya nchi hizo mbili uliofanyika jijini Oslo, Rais Samia alisema zipo kampuni kadhaa za Norway zilizotumia fursa hiyo vizuri kwa uchumi wa Tanzania.



Alisema kuwa kisiasa, Tanzania ina amani chini ya demokrasia imara ya mfumo wa vyama vingi, wenye kuzingatia tunu za utawala bora, kuheshimu haki za binadamu na utawala wa sheria.

Katika eneo la kijiografia, Rais Samia alisema Tanzania inafaa kwa uwekezaji hasa kutokana na kuwapo Bandari ya Dar es Salaam katika Bahari ya Hindi inayohudumia mataifa manane ya Afrika inayopakana nayo.

Kiuchumi, Rais Samia alisema Tanzania ina sera nzuri na imara za kifedha na kiuchumi na ukuaji wa Pato la Taifa uko kwenye asilimia 5.2 kwa mwaka na unatarajia kufikia zaidi ya asilimia sita mwaka ujao kama ilivyokuwa kabla ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Rais Samia pia alisisitiza fursa tano za kipaumbele; uwekezaji katika nishati mbadala, kilimo, mafuta na gesi, mifuko ya uwekezaji, miundombinu na usafirishaji.

Rais Samia amefanya ziara ya kitaifa ya siku mbili Norway baada ya kutoka kwenye ziara ya kihistoria Vatican, ambako alikutana na kufanya mazungumzo na Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
15.02.2024

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa kuanzia siku ya **Jumamosi tarehe 17-02-2024** hadi tarehe **20-02-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Kilombero kupitia Mikumi,** gari hizo zina namba za usajili: **T 807 DYL /T 877 EAU, T 164 DFC /T 390 DHQ, T 289 EDD /T 387 DHQ, T 116 EDS /T 310 DDH, T 914 DSD /T 572 EAZ**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 24.00**
   **Upana - mita 5.20**
   **Kimo - mita 5.20**

3. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi, gari zitasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

PUTO LA MUHIMBILI

# Apunguza kilo 55 ndani ya siku 385

**Na Christina Mwakangale**

VICENT Fortunatus, mkazi wa Mabibo-External, Dar es Salaam aliyewekewa puto tumboni Januari 23, mwaka jana ili kupunguza uzito wa kilo 150 aliokuwa nao, ndani ya siku 385, amepunguza kilo 55.

Jumatatu ya juma hili, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila ilimtolea puto ililomwekea, akiwa amepungua uzito kutoka kilo 150 hadi 95.

Bingwa wa Upasuaji na Mtaalamu wa Endoskopia katika hospitali hiyo, Dk. Edwin Muhondezi, alisema, "utoaji puto kwa Fortunatus umefanyika leo Februari 12 hapa hospitalini kutokana na muda wa kukaa na puto kwisha. (Puto) linaweza kudumu kwa muda wa miezi sita hadi 12," alifafanua Dk. Muhondezi.

Fortunatus, akielezea maendeleo yake kiafya, alisema kuwa sasa yuko vizuri. Sukari na presha viko sawa, hana tena changamoto ya maumivu ya mgongo iliyomsumbua awali na mwili wake sasa mwepesi, hata kuwa rahisi kwake kutekeleza majukumu kwa ufanisi.

Kwa mujibu wa takwimu za MNH - Mloganzila, hadi Oktoba, mwaka jana, takribani watu 150 walikuwa wamekewa puto katika tumbo la chakula hospitalini huko ili kudhibiti ulaji uliopitiliza. Hospitali hiyo ilianza kutoa huduma hiyo Desemba, 2022.



Baada ya kuwekewa puto / Kabla ya kuwekewa puto



Naibu Meya wa Jiji la Arusha, Joseph Mollel (kushoto) na Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Arusha, ASP Alijua Samut, wakimkabidhi cheti Sajini Taji Paul Kasambala, kwa mchango wake wa kusimamia Sheria ya Usalama Barabarani, katika hafla ya uzinduzi wa sare mpya za Chama cha Madereva wa Coaster mkoani Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Vijana 51,000 washiriki ujenzi SGR

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa tangu kuanza ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) mwaka 2017 hadi Desemba, mwaka jana, vijana Watanzania 51,153 wameshiriki katika utekelezaji wa mradi huo.

Naibu Waziri wa Ujenzi, David Kihenzile, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa anajibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Amina Ali Mzee.

Mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali kutoa ajira za kudumu kwa vijana ambao wanatumika kama vibarua kwenye ujenzi wa reli nchini.

Akijibu swali hilo, Kihenzile alisema kwa mujibu wa takwimu, tangu kuanza kwa ujenzi wa mradi wa SGR mwaka 2017, vijana hao wameshiriki ujenzi huo.

"Kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 1998, ajira katika utumishi wa umma huzingatia sifa na weledi na hutolewa kwa ushindani wa wazi.

"Hata hivyo, serikali inatambua kuwa vijana wanaoshiriki katika mradi wa ujenzi wa SGR wanapata ujuzi mahususi katika teknolojia ya reli ya kisasa ambayo itahitajika katika kuhakikisha uendelevu wa reli tunayoijenga," alisema.

Alifafanua kuwa kwa kuzingatia mahitaji ya uendeshaji reli, vijana hao watapewa kipaumbele kwa kuwa na sifa za ziada zinazohusiana na ujuzi waliopata kwa kushiriki katika ujenzi wa reli ya SGR pindi ajira hizo zitakapotangazwa.

# Dk. Slaa, Mwabukusi kushiriki maandamano ya CHADEMA leo

**Na Vitus Audax,** MWANZA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kinatarajiwa kuendelea na maandamano yake ya amani leo jijini Mwanza, ikiwa ni mwanzo wa awamu ya pili ya maandamano hayo katika majiji yote nchini.

Maandamano hayo yanafanyika licha ya taifa kuwa katika siku ya mwisho ya maombolezo ya siku tano ya kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu na Mgombea urais (CHADEMA) mwaka 2015, Edward Lowassa.

Akizungumza jana na Nipashe kuhusu maandalizi ya maandamano na mkutano na wananchi uliopangwa kufanyika kwenye viwanja vya Furahisha, Naibu Katibu Mkuu CHADEMA Tanzania Bara, Benson Kigaila, alisema maandamano hayo hayatasitishwa kutokana na msiba huo, bali msiba huo utakuwa sehemu ya kuenzi maisha ya Lowassa.

Kigaila alisema katika kutekeleza maandamano hayo, CHADEMA itakuwa inaeneza demokrasia aliyokuwa anaishi Lowassa kwa kuwa licha ya kifo chake, lazima chama kiendelee na kazi ya kutetea wananchi kupitia maandamano hayo na mkutano wa kuihimiza serikali kushusha gharama za maisha.

"Kifo cha ndugu yetu Lowassa ambaye anatambulika serikalini kama aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa Taifa hili, hakiwezi kutuzuia kuendelea na utetezi wa haki za Watanzania, bali tutafanya hivyo kwa kuyaenzi maisha yake na mazishi yake tutashiriki pia," alisema Kigaila.

Akithibitisha ushiriki wa viongozi wote wa chama hicho kitaifa, Katibu wa CHADEMA Kanda ya Victoria, Zakaria Obad, alisema kuwa katika maandamano hayo, aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa CHADEMA, Dk. Wibroad Silaa, Wakili Boniface Mwabukusi na Mwanaharakati Mdude Nyagali, maarufu Mdude CHADEMA, wanatarajiwa kuwa sehemu ya watakaoshiriki.

"Pia viongozi wote wa CHADEMA kitaifa wamethibitisha kushiriki katika maandamano na mkutano huu, hivyo niwakumbushe wafuasi na wasiokuwa wafuasi wa CHADEMA kushiriki kikamilifu maandamano haya kuishinikiza serikali kuweka mikakati ya kushusha hali ya maisha," alisema Obad.

Alisema katika maandamano hayo wanaishinikiza pia serikali kusikiliza maoni ya wananchi kuhusu miswada mitatu ya Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani pamoja na wa Sheria ya Vyama vya Siasa ambayo tayari imepitishwa na Bunge ikisubiri kutiwa saini na Rais.

Mwandishi wa habari hizi ameona nakala za barua zinazowapa rukhsa CHADEMA kuendelea na maandamano hayo kutoka ofisi za Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD) Nyamagana na Ilemela, pia nakala ya barua toka kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza.

# Mahakama yatoa amri nyumba mtoto wa Mbowe ipigwe mnada

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi imetoa amri na kumteua dalali wa kukamata nyumba ya mtoto wa Freeman Mbowe, Dudley Mbowe na kuipiga mnada kwa kushindwa kulipa Sh. milioni 62.7 za waandishi wa habari.

Uamuzi huo wa mahakama ulitolewa jana mbele ya Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Mary Mrio, baada ya kupitia hoja za washinda tuzo katika Tume la Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Julai 2023.

Shauri hilo Na. 28461 la mwaka 2023, linawahusisha wadai Maregesi Paul na wenzake tisa dhidi ya Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania Daima, Dudley Mbowe.

Akiwasilisha hoja mahakamani, Maregesi alidai Mkurugenzi Dudley baada ya wadai kushinda shauri, alikubali kulipa lakini baadaye hakutekeleza makubaliano.

"Amekaidi kutulipa, tumeona njia sahihi tumekubaliana tukamate nyumba yake Na. 9 iliyoko Mtaa wa Feza, Mikocheni B, Barabara ya Chipaka," alidai Maregesi.

Akitoa uamuzi, Naibu Msajili Mrio alisema mahakama inatoa amri ya kukamata nyumba namba tisa, iliyoko Mtaa wa Feza, Mikocheni B.

"Mahakama inatoa amri ya kukamata nyumba na imemteua Dalali wa Mahakama, Jesca Massawe kutoka Kampuni ya Udalali ya MM Auctioneer &Debt Collectors," alisema.

Baada ya uamuzi huo, mahakama iliahirisha shauri na kulipanga Machi 4, mwaka huu kwa ajili ya kupata taarifa ya utekelezaji amri hiyo.

Walalamikaji hao walipata tuzo Julai 17, 2023 mbele ya Mwenyekiti wa CMA, Bonasia Mollel.

Madai ya awali yalikuwa jumla ya Sh. milioni 114. Baada ya kukaa mezani kwenye majadiliano kwa pamoja, kiwango hicho cha fedha kilishushwa hadi kufikia Sh. milioni 62.7.

Dudley alikubali kulipa fedha hizo kwa awamu tatu, Oktoba 30 na Desemba 30, 2023 na awamu ya mwisho Februari 30 mwaka huu, lakini hajatekeleza makubaliano hayo.

Ilidaiwa na wadai kuwa katika kutafuta ufumbuzi wa suala hilo, Freeman Mbowe aliwaita wahariri wa Gazeti la Tanzania Daima ambao ni miongoni mwa wadai nyumbani kwa wakurugenzi wa Gazeti hilo, Dudley na Lilian Mtei.

Wahariri waliokutana na Mbowe Desemba 20 na 21, mwaka jana ni Maregesi, Fidelis Felix, Arodia Peter na Exuperius Kachenje. Inadaiwa kuwa katika majadiliano hayo, Mbowe alikubali kulipa madai ya wafanyakazi hao mwishoni mwezi Desemba mwaka jana, lakini hajatekeleza makubaliano hayo.

# Viwanda vya sukari kunufaika mabilioni kukabili hewa ukaa

**Na Romana Mallya**

VIWANDA vya sukari vinavyozalisha nishati safi ya umeme na kupeleka katika Gridi ya Taifa ni miongoni mwa wanufaika wa ruzuku ya Sh. bilioni mbili iliyotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) na Benki ya Maendeleo Tanzania (TIB).

Wanufaika ni wale wanaotekeleza miradi miwili inayohusu kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia na ule wa kurejeleza taka katika viwanda vinavyochakata nafaka za kilimo.

Mratibu wa Miradi Nishati na Mazingira wa UNIDO, Victor Hakimu, alisema lengo la miradi hiyo ni kulinda na kuboresha mazingira kwa kutumia taka kuzalisha nishati ya kupikia na ya umeme.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam katika hafla ya kukabidhi mfano wa hundi kwa wanufaika wa fedha za UNIDO, mratibu huyo alisema fedha hizo ni kwa viwanda vilivyofanikiwa kupata ruzuku za miradi hiyo miwili ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia na kurejeleza taka katika viwanda vinavyochakata nafaka za kilimo.

"Kama mlivyosikia kuna viwanda vingi vya sukari; Bagamoyo Sugar, Zanzibar Sugar, Kiwanda cha Sukari TPC, Manyara Sugar, wote hao wanafanya miradi ya aina mbili. Wanazalisha umeme kutokana na taka wanazozalisha kiwandani.

"Viwanda vimehamasishwa katika kufanya shughuli ambazo zote zinalenga kulinda mazingira. UNIDO inafanya mradi huu pamoja na TIB na wadau wetu serikalini ambao ni Wizara ya Nishati, Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira," alisema.

Alitaja wafadhili wakubwa wa miradi hiyo kuwa ni Bara la Ulaya na Mfuko wa Nishati wa Dunia.

Mkurugenzi wa Mipango na Biashara wa TIB, Joseph Chilambo, alisema kwa kushirikiana na UNIDO wametoa hundi kwa wadau mbalimbali saba wanaojishughulisha miradi ya kupunguza hewa ukaa angani.

"Tunajua matumizi ya kuni na matumizi ya nishati ambazo si safi siyo tu yanachafua mazingira, bali husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira kwa kukata miti.

"TIB na UNIDO tumekuja na mpango huu wa majiko mapya yanayotumia nishati safi inayotokana na mabaki ya mazao," alisema.

Pia alisema hiyo ni fursa kwa viwanda kwa kuwa ili watengeneze nishati inabidi watengeneze viwanda, hivyo wametoa fedha kwa wafanyabiashara hao kuanzisha viwanda vya kutengeneza mafuta ya ethanol.

"Ufadhili huu kwa jumla ni wa Sh. bilioni mbili. Kati ya hizo Sh. bilioni moja zinakwenda katika viwanda kusaidia kuandaa miradi. Wataandaa maandiko yatakayopelekwa benki na taasisi zingine za fedha ili kupata mitaji ya kujenga viwanda," alisema.

Aliongeza kuwa fungu lingine ni kwa kampuni zinazouza majiko safi, lengo watengeneze majiko zaidi na kusambaza kwa bidii.

Ofisa Mtendaji Utawala Kiwanda cha Sukari TPC, Jaffary Ally, alisema kiwandani huko wanazalisha sukari na hutumia mabaki ya miwa kuzalishia nishati ya umeme.

"TPC kwa muda wa miaka 17 tunazalisha umeme megawati 17.5. Kwa matumizi ya ndani tunatumia megawati 13 na kiwango kinachobaki tunakipeleka kwenye Gridi ya Taifa, tunauzia umeme safi Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)," alisema.

"Ruzuku tuliyopata leo (jana) kutoka UNIDO itatumika kuwekeza mitambo mingine. Tulikuwa tukipeleka katika Gridi ya Taifa megawati tatu hadi nne. Sasa tutazalisha kiwanda kingine na kuongeza megawati hadi kufikia 7.5 kwenda katika Gridi ya Taifa.

"Tunaamini huu ni mchango mkubwa kusaidia upatikanaji wa nishati safi na salama katika Gridi ya Taifa. Mwezi huu (Februari) tutaagiza mitambo nje ya nchi na tunatarajia mwezi Aprili, mwaka huu, itakuwa imewasili TPC na ujenzi unatarajia kuchukua miezi 18. Hadi mwaka 2025 tutakuwa tumeanza uzalishaji wa umeme mwingine," alisema.

Ally aliomba Wizara ya Nishati itengeneze mazingira rafiki kwa kuwa viwanda vingi vya sukari vina uwezo wa kuzalisha nishati na kuupeleka katika Gridi ya Taifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Consumer's Choice, Limited, Frida Mlingi, alisema wana dhamana ya kusambaza majiko yanayotumia nishati safi kwa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na Mwanza.

Alisema wana dhamana ya kusambaza majiko 6,000 kwa miezi 17 kuanzia Agosti mwaka jana mkoani Dar es Salaam na mradi mwingine unahusu majiko 20,000 kwa kipindi cha miezi 16 mkoani humo.

"Fedha hizi zitatumika vizuri kwa sababu wametuwezesha sisi pamoja na wateja wanaotumia mkaa na kuni ambao sasa watapata jiko kwa bei nafuu na mafuta yatapatikana karibu na wao," alisema.


Kamal

**KAMAL GASES LIMITED**

**TAARIFA KWA UMMA**

Sisi **Kamal Gases limited** wazalishaji namba moja wa gesi za viwandani zenye ubora uliothibitika na Shirika la viwango Tanzania TBS.

Tumegundua kuwepo kwa wazalishaji wa gesi wanaotumia mitungi yenye nembo ya KGL kinyume na sheria.

Tunawatangazia wazalishaji, watumiaji wa gesi za viwandani na umma kwa ujumla kwamba ni kinyume cha sheria kujaza, kuuza, na kusambaza gesi iliyowekwa kwenye mitungu yenye nembo ya kamal ambayo haikuzalishwa na Kamal Gases Limited.

Hivyo mnahabarishwa kwamba; Kamal Gases Limited wapo katika zoezi kabambe la kufuatilia na kukamata wahusika wote wanaozalisha gesi za viwandani na kujaza katika mitungi yenye nembo au alama ya kamal gases limited kinyume cha utaratibu.

Kamal Gases Limited itachukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufungua kesi za madai na jinai kwa yoyote atakaye tumia mitungi ya gesi yenye nembo ya Kamal Gases Limited kujaza gesi aliyoichakata mwenyewe au iliyochakatwa na wazalishaji wengine nje ya Kamal Gases Limited

Tunatoa wito kwa wateja wetu kuendelea kutumia huduma ya gesi ya Kamal Gases Limited kwa kupitia vituo vilivyoidhinishwa na kuitambulika na Kamal Gases Limited au wafike kiwandani chang'ombe industrial area plot no. 188/2 kwa maelezo zaidi piga simu namba **+255 765 169 444**

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Kamal Gases Limited**
**Dar es Salaam**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ujumbe TEC kuhusu Kwaresma ufundishe viongozi kutenda haki

**WAKRISTO** duniani, jana walianza rasmi siku 40 za majira ya Kwaresma ikiwa ishara ya Mwokozi wao Yesu Kristo alipoyaendea mateso kabla ya kukamatwa, kusulubiwa na kuangikwa msalabani hatimaye kufa. Kwa baadhi ya madhehebu, hiki ni kipindi cha kufungwa kwa siku 40 kama Yesu Kristo alivyofunga kabla ya kujaribiwa na ibilisi na hatimaye kuyashinda majaribu.

Pamoja na kwamba ni majira ya kufunga, kwa wengi ni kipindi ambacho hutafakari maisha yao huku wakitakiwa kuyaishi na kutenda mambo mema mfano wa maisha aliyoyaishi Yesu Kristo katika muda aliokaa duniani. Pia hutakiwa kutafakari ni mahali gani walipoanguka na kutengeneza ili kuishi maisha matakatifu na ya kumpendeza Mwenyezi Mungu.

Kwa mantiki hiyo, kwa wale wanaofuata na kuyaishi maisha ya Ukristo kama ipasavyo, wanatakiwa kuwa watu wema kwa jamii na kufanya matendo mema. Pia ni kipindi cha kumrudia Mwenyezi Mungu na kutenda matendo ya huruma kwa makundi yenye uhitaji kama vile wagonjwa, yatima, wajane na wafungwa.

Kutokana na umuhimu wa Kwaresma, Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania (TEC) limetoa ujumbe wa unaosisitiza masuala mbalimbali yakiwamo imani, maadili, siasa, utamaduni, tunu za kiutu, uchumi na mazingira huku ukitiwa saini na maaskofu 38, wakiwamo Rais wa Baraza hilo, Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga wa Jimbo Kuu la Mbeya na Mwadhama Protase Kardinali Rugambwa, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Tabora.

Mambo mengine yaliyosisitizwa ni umuhimu wa mtu kuongozwa ili kufikia wongofu pamoja na ujasiri na unyenyekevu. Msisitizo mkubwa katika maeneo hayo ni kiongozi kuwa jasiri katika kukabili tatizo huku akiwa na unyenyekevu wa kufanya yote kwa upendo, hivyo kukubalika na watu anaowaongoza.

Jambo lingine lililogusiwa katika ujumbe huo ni wajibu wa familia na kanisa katika eneo la malezi, ili kuandaa viongozi wazuri wenye sifa stahiki kwa imani kwamba kama hilo halitatimizwa, kuna uwezekano mkubwa wa kupata viongozi wasio na sifa. Kwa kufanya hivyo, matokeo yake ni kupata viongozi wasio na sifa huku nguvu na fedha (rushwa) vikichukua nafasi.

Aidha, imehimizwa kwa viongozi kuwa na kwa watu wanaowaongoza na kuwasaidia kadri wawezavyo. Pia imesisitizwa wale wanaoongozwa wawe wanyenyekevu wa kusikia na kutii sauti ya viongozi wao pamoja na ujasiri wa kuuliza, kukubali kukosolewa, kusahihishwa na kurekebishwa.

Sambamba na hilo, wenye mamlaka wamepewa somo kuhusu kuyafumbia mambo yanayokwenda kinyume cha maadili pamoja na kuwapo kwa vitendo vinavyokiuka haki na usawa katika jamii pamoja na kuwapo kwa wizi, ukwepaji kodi, rushwa, ufisadi na magendo.


Mambo hayo yaliyoelezwa na viongozi hao wa kanisa kubwa na lenye wafuasi wengi zaidi duniani, yanalenga maisha ya kila siku ya mwanadamu na yale ambayo yanmekuwa yakitendeka siku kwa siku. Kila mtu (mtawala na mtawaliwa) amepewa sehemu yake ya kujitafakari na na kuyaishi maisha yenye kielelezo halisi cha Ukristo.


Iwapo yote hayo yatatendeka huku kila mtu akiwa na hofu ya Mungu katika kila neno na tendo, ni wazi kwamba amani, upendo, umoja na mshikamano miongoni mwa Watanzania, vitatamalaki huku jamii ikiishi kwa usawa bila manung'uniko.

Viongozi wanapaswa kutenda yawapasayo kwa kutenda haki dhidi ya wanaowatawala badala ya kutanguliza maslahi binafsi kwa kujilimbikizia mali huku wananchi wakipata shida kwa kukosa huduma mbalimbali za muhimu.

Wananchi nao wanapaswa kutimiza wajibu kwa kufanya kazi, kuwa na unyenyekevu, ujasiri wa kuhoji bila woga yale yanayofanyika kinyume na kufichua maovu. Vyombo vilivyopewa mamlaka katika kutekeleza sheria na kutoa haki, navyo vitende kadri vinavyopaswa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# Tuwasaidie wenye ulemavu kupitia falsafa, nao ni sehemu ya jamii yetu

Na Tuntule Swebe

**JAMII** nyingi za Kiafrika bado hazijapata elimu ya namna ya kumsaidia mwenye ulemavu. Imekuwa kawaida sana wenye ulemavu kuwekwa barabarani na kuanza kuomba chochote kitu kwa wapita njia.

Ni hali inayoonekana kuzoeleka sana, kwani watu hao wanakalishwa barabarani tena bila ya huruma. Baadhi ya barabara hizo mkoani Dar es Salaam, ni Mwenge, Kariakoo, Tegeta na sehemu nyingine nyingi.

Jambo hilo hufanyika wakikalishwa njiani nyakati zote, iwe mvua, jua hata baridi. Watu hawa wanawaweka sehemu moja kwa hali yoyote wawe wazima, wanaumwa, wamechoka na hata kama hawajachoka. Jambo hili limeleta sintofahamu kwa jamii.

Kwa kuwa ni kawaida wanatumikisha pasipo kujali kabisa afya zao wao wapo kimaslahi, mwanadamu yeyote lazima ukumbuke kesho yako huishi kwa kutafakari.

Je, hicho kinachofanyika ni haki kwa binadamu? Je, kama ungelikuwa wewe unapitia hayo, ungejisikiaje katika sheria za nchi? Pia katika ubinadamu wako ukitetea haki zako za msingi.

Tuelewe, mtu anapoenda kinyume na haki za mwingine, unastahili kupewa adhabu kali, maana kitu chochote ambacho kwako hupendi kufanyiwa, anapofanyiwa mwingine, nayo ni mbaya.

Wote mbele ya uso wa dunia, hatujui kesho ikoje, kwani ikumbukwe kuwa wenye ulemavu wengi sio kwamba wamezaliwa nao, bali wengine wamepata kwa ajali au magonjwa.

Yapo mashirika yanayowatetea wenye ulemavu, mfano mojawapo ninalifahamu, ikitamka watu wenye ulemavu wana haki kama mtu mwingine na wanahitaji msaada wa matibabu katika hali yoyote.

Ilitamkwa katika Siku ya Wenye ulemavu Duniani, malengo yake ni kuwapa waliopo na ulemavu kuwa na haki zao.

Hata hivyo, kwenye nafasi ya uchumi mwenye ulemavu ana haki na hiyo ipo sana katika nchi kama Marekani. Daima mtoto huyo anapewa nafasi na mazingira kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kiuchumi katika jamii.

Ni vizuri tukaiga huko, tunawatetea wenye ulemavu na tunawasaidia. Hiyo inajenga upendo na hamasa kwa watu wengine.

Hata watoto wanapokuwa na maadili ya kusaidia na kuwapenda wenye ulemavu, mmoja ya walio mfano wa kuigwa katika hilo ni marehemu Dk.Reginald Mengi, aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa kampuni ya IPP.

Huyo aliweza kuonyesha upendo kwa wenye ulemavu na kuwaonyesha watu dhahiri kuwa wenye ulemavu wana haki kama watu wengine.

Kwa vitendo, akafanya sherehe kila mwaka akijumuika nao, kwa chakula cha pamoja. Ni hali inayokuimbusha ukweli kwamba, 'mlemavu ana haki kama mtu mwingine yeyote'.

Dk. Mengi akaonyesha usawa, kwani aliwapatia watu ajira wenye ulemavu.

Kuna baadhi ya jamii wana dhana au falsafa kinyume, wakiwasumbua sana katika jamii zao kama vijiji, wakiwatenga wenye maradhi kama ya ukoma.

Niwakubushe wahusika kokote waliko, kwam, na uhalisi uko kinyume nao katika dhana ya jamii hizo wakihisi 'wamelaaniwa. Nataka kuwahakikishia wenye ulemavu wana haki na sura zote za binadamu wa kawaida, kasoro magumu ya kimaumbile kibinadamu.

Hata hivyo, kuna baadhi walio mjini na vijijini wanawatenga. Ila ukweli, hata mwenye ulemavu ana haki ya kuishi, pia baadhi ya waganga wa jadi wamegubikwa na kiza hicho.

Wanadhani hali ya mtu kuwa na kasoro ya viungo au baadhi ya sehemu za mwili kuwa kasoro kama ngozi, wanageuza ni sehemu ya kutenda yaliyo kinyume na utajiri katika 'njia pori.'

Wengine wanajiwekea dhana, kuwa watu hao wenye ulemavu ni mikosi na laana kitaifa.

Ukweli upo; watu wote ni sawa na wanahaki kama wengine. Dhana, fikra za laana, mikosi na umaskini havitokani na kuwapo kwa watu hao.

Sasa basi, kwenye daladala abiria na dereva, pia makondakta wanapaswa kupeana elimu ya kuwasaidia wenye ulemavu, ushirikiano kama kuwapisha wakae kwenye viti, ni sehemu ya uungwana.

# Duni, Othman kupimana ubavu uenyekiti wa ACT

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI Taifa wa ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji, amechukua fomu kutetea kiti chake huku wenyeviti na makatibu wa chama hicho wa mikoa 25 nchini wakijitokeza kumchukulia fomu Makamu Mwenyekiti, Othman Masoud Othman ili awanie nafasi hiyo.

Kwa sasa Othman Masoud ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar na Makamu Mwenyekiti Taifa wa ACT-Wazalendo, ambaye wenyeviti na makatibu hao wamesema wanakwenda kumwomba awanie nafasi hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kiza Mayeye aliyeongoza jopo hilo la wenyeviti na makatibu, alisema licha ya kutambua juhudi kubwa za ujenzi wa chama zilizofanywa na Duni wakati wa uongozi wake, kwa sasa wanaona ni wakati mwafaka kwa Othman kuongoza chama hicho.

"Chama chetu kina watu wengi wenye uwezo wa kushika nafasi ya uongozi. Wakati huu wa uchaguzi tumeona kuna haja kuwa na nguvu mpya na kwa maoni yetu tumesema tukamwombe makamu wetu apande juu na kesho (leo) tunakwenda Zanzibar kuomba akubali ombi letu," alisema Mayeye.

Alisema Othman kwa maoni yao, atakisogeza chama mbele zaidi ya mwenyekiti wa sasa na wanatarajia hatawakatalia ombi lao la kuwania nafasi hiyo.

"Imani yetu ni kwamba hili tumelianzisha sisi tuliopo hapa, lakini na wajumbe wengi wa mkutano mkuu wanaunga mkono hatua hii na watazunguka kumtafutia kura ndugu Othman na tukishamkabidhi fomu tutarudi katika mikoa yetu kumtafutia kura na tutahakikisha anakuwa Mwenyekiti wa Chama Taifa," alisema.

Naye Duni, mwenyekiti anayemaliza muda wake, ameshajitokeza visiwani Zanzibar kuchukua fomu ya kutetea nafasi hiyo.

Awali Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya ACT Wazalendo, Joran Bashange, alisema wamefungua rasmi uchukuaji fomu na kuanzia sasa kila aliyechukua fomu anaruhusiwa kufanya kampeni bila kujeruhi sifa za wagombea wengine.

Alisema uchaguzi wa chama hicho utaanza kwa ngome za chama kuchagua viongozi wake na kutaja kuwa uchaguzi wa ngome ya vijana utafanyika Februari 29, wakati ngome ya wazee uchaguzi wao utafanyika Machi Mosi huku ngome ya wanawake wakichaguana Machi 2, mwaka huu.

Nafasi ya viongozi wakuu wa kitaifa zitakazowaniwa ni Kiongozi wa Chama, Mwenyekiti na Makamu wake wawili kutoka pande mbili za Muungano.

Nafasi zingine ndani ya chama hicho ni pamoja na wajumbe 24 wa Kamati Kuu na wengine 24 wa Halmashauri Kuu. Uchaguzi wa nafasi ya kiongozi wa chama utahitimishwa tarehe Machi 6, mwaka huu.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Fahari wakishiriki na wenzao wa Shule ya Sekondari Kiluvya kwenye mjadala wa hadhara wakati wa mashindano ya usomaji vitabu na mijadala kuchambua maudhui wenye lengo la kuhamasisha tabia ya usomaji vitabu, yaliyodhaminiwa na PROBONO katika Wilaya ya Ubungo Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya TIB taabani, yashindwa kujiendesha

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

HALI mbaya ya ukwasi na ukata wa mtaji, unaipitisha kwenye tanuru la moto Benki ya Maendeleo Tanzania (TIB), hivyo kuifanya kushindwa kujiendesha huku ikipata hasara ya Sh. bilioni 129 kutokana na mikopo chechefu iliyofikia asilimia 20.

TIB inashindwa kujiendesha na kukidhi masharti ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kutokana na kuwa na mtaji wa Sh. bilioni 24 pekee, ilihali kiwango cha chini cha kuruhusiwa kuendelea ni Sh. bilioni 200.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) iliyosomwa Bungeni Dodoma jana na Mwenyekiti wake, Deus Sangu, TIB imeshindwa kulipa amana ya Sh. bilioni 206.8 zilizowekwa na watu na taasisi za serikali.

Katika taarifa hiyo, Bunge limeelezwa kuwa benki hiyo imepata hasara ya Sh. bilioni 129 kwa miaka miwili mfululizo kati ya mwaka 2021 na 2022.

Sangu, ambaye ni Mbunge wa Kwela, alisema amana hizo zimefika muda wa kurejeshwa lakini kutokana na hali mbaya ya ukwasi, benki imeshindwa kuzirejesha.

"Kimsingi, hasara kubwa imepatikana mwaka 2022 ambayo ni Sh. bilioni 195.91. Hasara hii ilitokana na kuongezeka kwa lengo la mikopo chechefu hadi asilimia 20, sawa na Sh. bilioni 159.73 wakati ukomo uliowekwa na BoT ni asilimia tano.

"Kwa ujumla, TIB ina hali mbaya na kwa kuzingatia umuhimu wa uwapo wa benki hii, ni rai ya kamati kwamba, jitihada za makusudi zinapaswa kuchukuliwa ili kuiwezesha kupata mtaji toshelevu.

"Pamoja na hilo, TIB inahitaji mifumo imara ya uendeshaji wa shughuli za benki, hususani mfumo wa uchakakataji maombi ya mikopo na ufuatiliaji ili kuiwezesha benki kutozalisha mikopo chechefu mingine," alisema Sangu.

**MZIGO SI WAKE**

Aidha, Bunge limeelezwa kwamba TIB inaendesha dirisha la kilimo, jukumu ambalo linaendana na jukumu la msingi la Benki ya Maendeleo ya Tanzania (TADB). Pia imekabidhiwa majukumu mengine mengi ambayo kimsingi si sehemu ya jukumu la msingi la benki hiyo.

Mwenyekiti huyo alifafanua kuwa majukumu hayo ni pamoja na usimamizi wa mradi wa kuendeleza na kusambaza nishati jadidifu Tanzania (TEDAP) na mradi wa usambazaji wa majiko yanayotumia nishati mbadala kwa ajili ya kupunguza matumizi ya mkaa.

Mengine ni mashamba ya maua (Arusha), mradi wa upanuzi wa Nishati ya Umeme Vijijini (TREEP) na mradi wa kuchagiza matumizi ya umeme jua katika kusukuma maji katika Jumuiya za watumia maji vijijini.

Mengine ni kiwanda cha kusindika nyama kinachomilikiwa na kampuni ya Sumbawanga Agricultural and Animal Food Industries (SAAFI) na iliyokuwa Benki ya Nyumba Tanzania (THB).

Kutokana na benki hiyo kushindwa kujiendesha, Bunge limeazimia serikali ifanye tathmini kubaini umuhimu, uendeshaji na ustahimilivu wake ili kuchukua hatua stahiki.

Pia limeitaka serikali iisimamie na kuhakikisha, TIB inajielekeza kutekeleza majukumu yake ya msingi, bila kuendelea na shughuli zilizo nje ya malengo ya kuanzishwa kwake na serikali isimamie kwa dhati na kufuatilia kwa karibu wadaiwa sugu ili kulipa madeni yao kwa lengo la kuongeza ukwasi wa benki hiyo.

Azimio lingine la Bunge ni kuitaka serikali ihakikishe kuwa amana zinazodaiwa na watu binafsi na taasisi za serikali yanalipwa ili kupunguza madhara kwa wadai au taasisi hizo.

**KABWELA** FADHILI MOHAMED





Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dk. Athuman Ngenya (katikati), akifungua mkutano wa wadau wa unga wa mahindi na siagi ya karanga, katika ofisi za shirika hilo, Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Tanzania yaandika historia mkutano wa Rais Samia, Papa Francis Vatican

## •Ni mwendelezo wa alichoasisi Nyerere 1979

**Na Mwandishi Maalum**

ZIARA ya kikazi ya Rais Samia Suluhu Hassan Vatican tarehe 10-12 Februari, mwaka huu, imedhihirisha ustadi wa diplomasia, Tanzania ikiandika historia kwa mara nyingine tena kupitia mkutano huo wa Rais Samia na Baba Mtakatifu Francis.

Katika mkutano wa viongozi hao uliodumu kwa takriban dakika 25, viongozi hao walishiriki kwenye mazungumzo ya faragha na mazungumzo ya wazi, ambayo yaliashiria dhamira kuu ya pamoja ya kutangaza amani, umoja na mshikamano duniani na ushirikiano wa kidiplomasia baina ya Tanzania na Vatican.

Ingawa ni desturi kwa Papa kupokea viongozi wa dunia, mapokezi ya Rais Samia Vatican yameingia kwenye historia, yakiakisi Rais mwanamke wa kwanza Tanzania kuzuru Vatican na mchango wa mawazo kati ya viongozi hao kutoka asili na tamaduni tofauti.

Kwa mujibu wa taarifa rasmi kutoka Ofisi ya Papa Francis Vatican, mazungumzo ya viongozi hao yaliyotawaliwa na urafiki na heshima, yalisisitiza maono ya pamoja ya kukuza uelewa mpana zaidi katika jamii yenye mchanganyiko wa dini na kuendeleza umoja katika kuleta maendeleo ya pamoja.

Kwa mara ya kwanza kutokea Tanzania, ujumbe wa Rais Samia kwenye ziara hiyo ulijumuisha viongozi muhimu kutoka jamii ya Kikatoliki ya Tanzania ukiwakilisha waumini wa kawaida kabisa wa kanisa hilo linaloongoza kwa ukubwa Tanzania. Miongoni mwao ni Prof. Deogratias Rutarora, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Walei Taifa; Dalmas Gregory, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Walei - Zanzibar; Evaline Malisa Ntenga, Mwenyekiti wa Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) na Rais wa Wanawake Wakatoliki Afrika; Leonard Ibrahim Mapolu, Mwenyekiti wa Vijana Wakatoliki Wafanyakazi Tanzania (VIWAWA); na Theresia Paskasi Seda, Mwenyekiti wa Utoto Mtakatifu wa Papa, Jimbo Kuu la Dar es Salaam.

Ushiriki wa wawakilishi hao pamoja na wasaidizi wa Rais Samia, si tu ishara ya umuhimu wa mazungumzo ya kidini bali pia ni kudhihirisha tena dhamira ya Tanzania ya kukuza ushirikiano kati ya taasisi za kidini na serikali.

Zaidi ya ujumbe uliombatana na Rais Samia, mazungumzo yake na Papa Francis yamelenga kuimarisha zaidi uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na Vatican, na kufungua milango ya ushirikiano kwenye maeneo muhimu kama elimu, huduma za afya, na juhudi za amani na ulinzi wa amani duniani.

Uhusiano wa kihistoria kati ya Tanzania na Vatican ulianza rasmi baada ya Ubalozi wa Vatican kufunguliwa jijini Dar es Salaam mwaka 1968. Ni uhusiano kati ya mataifa hayo mawili uliowezesha ushirikiano wa kidugu ambao ni endelevu unaotegemea maadili na maslahi ya pamoja. Chini ya uongozi wa Rais Samia, Tanzania imeweka kipaumbele kwenye upatikanaji elimu bora na huduma za afya kulingana na malengo ya Kanisa Katoliki ya kuhudumia watu.

Miradi ya serikali chini ya uongozi wa Rais Samia kama vile kuendelea na Mpango wa Utoaji Elimu msingi Bila Malipo 'elimu bure' na ujenzi wa vituo vya afya na maboresho ya huduma za afya, inaonyesha dhamira ya dhati ya Rais huyo kuleta maendeleo na ustawi kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Wakati Watanzania na waumini wa Kanisa Katoliki duniani wakiendeleea kutafakari umuhimu wa ziara hiyo, ni dhahiri kwamba ziara ya Rais Samia Vatican inawakilisha zaidi ya mazungumzo ya kidiplomasia. Ni uthibitisho wa dhamira ya Tanzania ya kuendelea kukuza amani na ushirikiano wa kimataifa.

Ziara ya kihistoria ya Rais Samia Vatican inaendeleza utamaduni wa ziara na mazungumzo ya kidiplomasia kati ya Tanzania na Vatican, kama ilivyoanzishwa na marais watangulizi isipokuwa Hayati Rais John Magufuli, aliyefariki akiwa madarakani Machi 17, 2021.

Mwaka 2012, Rais Jakaya Mrisho Kikwete alizuru Vatican, alifanya mazungumzo na Papa Benedict juu ya masuala ya ushirikiano kati ya Vatican na Tanzania ikiwamo kudumisha amani. Vivyo hivyo, mwaka 2005, Rais Benjamin William Mkapa alishiriki mazungumzo na Papa Benedict wakati wa ziara yake ya Vatican.

Wakati wa utawala wa Rais Ali Hassan Mwinyi mwaka 1989, Tanzania ilimkaribisha Baba Mtakatifu John Paul II, katika ziara kubwa iliyojumuisha mikoa mitano tofauti. Ratiba ya Papa ilijumuisha mikoa ya Dar es Salaam, Ruvuma, Tabora, Mwanza na Kilimanjaro. Ziara hii ya kihistoria ilionesha ukarimu wa Tanzania na pia ilionesha umuhimu wa nchi ya Tanzania katika jukwaa la kimataifa.

Vilevile, ziara hii ilionesha utamaduni wa Tanzania na kujenga umoja wa kitaifa usiojali tofauti za kidini, kukuza mazungumzo na ushirikiano na viongozi wa kidini.

Mbali na ziara ya Baba Mtakatifu John Paul II, historia ya kidiplomasia ya Tanzania na Vatican inaonesha kuwa mwaka 1979, Rais Julius Nyerere alifanya ziara muhimu Vatican. Kwenye ziara hiyo aliambatana na Sheikh Thabit Kombo (marehemu), aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Afro-Shirazi cha Zanzibar.

Katika mkutano huo wa kihistoria, Sheikh Kombo aliheshimiwa kwa medali na Papa John Paul II, akithamini mchango wake wa thamani kwenye uongozi wa visiwani Zanzibar uliofanikisha amani na Muungano wa Tanzania.

Ziara hizo zilizofuatana zinaonesha dhamira endelevu ya Tanzania katika kukuza uhusiano wa kidiplomasia na Vatican na kuthibitisha umuhimu wa mazungumzo na ushirikiano kati ya pande zote mbili yenye kudumisha ushirikiano wa kidiplomasia.

Mkutano wa hivi karibuni wa Rais Samia na Papa Francis unajenga urithi huo, ukiimarisha zaidi uhusiano kati ya Tanzania na Vatican na kuweka njia ya ushirikiano endelevu katika maeneo yenye maslahi na manufaa ya pamoja.

# Waja na mkakati kupunguza uzalishaji wa kaboni nchini

**Na Frank Monyo**

UMOJA wa Wafanyabiashara wa Gesi ya Mitungi ya Majumbani (TZLPGA) umesema umedhamiria kupanua matumizi ya teknolojia ya gesi majumbani na kupunguza uzalishaji kaboni, ili kurahisisha upatikanaji nishati safi ya kupikia.

Juzi Mkurugenzi Mkuu wa umoja huo, Amos Jackson aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuwa umoja huo ulioanzishwa mwaka 2023, unaundwa na kampuni sita zinazofanya biashara ya gesi za mitungi kwa matumizi ya majumbani ambazo ni CAMGAS, O-GAS, LAKE GAS, TAIFA GAS, ORYX GAS, MANJI GAS na PUMA ENERGY.

"Tunaamini kuwa ukusanyaji na usambazaji taarifa sahihi kwenye sekta hii utasaidi kuleta mageuzi makubwa kwenye kufanikisha azma ya nchi yetu kupiga hatua kwenye matumizi ya gesi za mitungi majumbani.

"Kwahiyo, kuwapo kwenu waandishi wa habari hapa katika mdahalo wetu kutasaidia sana kupanua ufahamu wetu kupitia maoni yenu kama wadau muhimu wa sekta hii," alisema.

Mwenyekiti wa TZLPGA, Benoit Araman alisisitiza kuhusu umuhimu wa kudumisha ushirikiano baina ya wadau wa sekta hio na serikali.

Alisema: "Ni wajibu wetu kuiunga mkono serikali kuhakikisha tunaleta mapinduzi kwenye sekta hii ya gesi majumbani ili kutokomeza uharibifu wa mazingira unatokana na matumizi ya mkaa.

"Mkaa ni tishio kwa maana huchangia kutengeneza hewa ya kaboni ambayo inachafua mazingira na kuleta mabadiliko hasi ya tabianchi," alisema Araman

Mdahalo huo uliohudhuriwa na mgeni rasmi, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Dk. James Andilile ambaye aliunga mkono uzinduzi wa kampeni wa kusambaza taarifa sahihi juu ya matumizi salama ya gesi (LPG) kwa manufaa ya taifa kwa ujumla.

TZLPGA iliahidi kushirikiana na wadau wa sekta hio kutoa msukumo wa wawekezaji kutoa fedha kwa ajili ya kukuza matumizi ya nishati safi na athari zingine chanya zitakazosaidia kuwa na tija katik sekta ya nishati kwa ajili ya maendeleo ya taifa zima.



## Watoto 27,431 kupata kinga ya surua

**Na Steven William,**
MUHEZA

WATOTO 27,431 wanatarajiwa kutapatiwa chanjo ya kinga ya ugonjwa wa surua na rubella wilayani hapa Mkoa wa Tanga hivi karibuni.

Hayo yalisemwa jana na Mratibu wa chanjo Wilaya ya Muheza, Grace Mwaimu katika Kikao cha Kamati ya Afya ya Msingi.

Dk. Mwaimu alisema kuwa Muheza imepokea dozi za chanjo hiyo 27,431. Kauli mbiu ya chanjo hiyo kwa mwaka huu ni Onesha Upendo Mpeleke Mtoto Akachanjwe.

Alisema dawa hizo zimesambazwa katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya katika wilaya hiyo.

Alisema kampeni hiyo ina lengo la kutoa chanjo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kwamba itafanyika kwa utaratibu kwenye vituo vyote vya afya, maeneo yenye mikusanyiko ya watu kama vile vituo vya mabasi, sokoni na minadani.

"Nitoe wito kwa wajumbe katika uhamasishaji wananchi kupeleka watoto wao kupata chanjo," alisema Mwaimu.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Dk. Juma Mombokaleo, aliwataka wanahabari, viongozi wa jamii, dini na wadau wengine kuhakikisha ujumbe unawafikia walengwa kwa uhakika na kwa wakati.

Dk. Mombokaleo, alisema Muheza imejipanga kutekeleza kampeni hiyo muhimu kwa afya za watoto na jamii ya kama ambavyo serikali imeelekeza.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Mohamed Mfaki, alisema uzinduzi wa kitaifa wa kampeni ya siku tano kilele chake ni Februari 18, mwaka huu.

**Dk. Mwaimu alisema kuwa Muheza imepokea dozi za chanjo hiyo 27,431. Kauli mbiu ya chanjo hiyo kwa mwaka huu ni Onesha Upendo Mpeleke Mtoto Akachanjwe.**

# Tanzania yaombwa kupitia adhabu ya kifo

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MAHAKAMA ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR) imetoa ombi kwa Tanzania kupitia upya sheria ya adhabu ya kifo kwa watuhumiwa wanaopatikana na hatia ya mauaji ili kuwapa wigo majaji wa kuchagua adhabu kulingana na uzito na mazingira ya kesi.

Ombi hilo lilitolewa jana jijini Arusha mbele ya jopo la majaji tisa likiongozwa na Rais wa Mahakama ya Afrika, Jaji Imani Aboud, katika kesi hizo tatu zilizofunguliwa awali na wafungwa wa Tanzania waliohukumiwa adhabu ya kifo kwa kosa la mauaji. Katika maamuzi ya usikilizwaji wa kesi hiyo chini ya jopo la majaji hao wa mahakama hiyo yenye makao yake makuu jijini Arusha, yameainisha jinsi majaji wa Mahakama ya Tanzania walivyofungwa mikono na sheria.

Majaji hao wa nchini, hawana chaguo mbadala la adhabu kwa mtu aliyethibitika kufanya kosa la mauaji bali ni adhabu ya kifo pekee.

Naibu Msajili wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Grace Kakai, alisema katika hukumu za vifo zinazotolewa na mahakama ya Tanzania, hazitoi adhabu mbadala kama vile kifungo cha muda mrefu badala yake ni kifungo cha maisha.

"Tunaomba Wizara ya Katiba na Sheria ichapishe hukumu zetu katika tovuti zao ili wananchi nao wazisome na kujua mahakama hii inafanya nini katika uendeshaji wa kesi zake," alisema.

Wakili wa Mahakama Kuu, Baraka alisema hukumu zinazotolewa zinaambatana na maelekezo ya kipindi maalumu cha utekelezaji na ni hatua nzuri inayothibitisha utii wa Tanzania kusimamia itifaki na mikataba ya kimataifa iliyoridhia.

Watu hao watatu waliohukumiwa kifo na Mahakama Kuu Tanzania katika kesi tofauti zilizothibitishwa na Mahakama ya Rufani na badaye kukata rufani katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu ni Deogratias Nicholas, Crospery Gabriel na Ronald William.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdalla, akiendesha harambee ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Kibaya, Kata ya Misima, wilayani Handeni hivi karibuni, baada ya kuzindua tawi la kikundi cha wanawake wajasiriamali kijijini humo. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# EAC kujiimarisha soko la dunia

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUSHA

NCHI Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zimekubaliana kuimarisha ushirikiano wao katika biashara na uwekezaji ili kukabiliana na ushindani katika soko la dunia.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuushiriki Mkutano wa Baraza la Mawaziri la Kisekta wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji (SCTIFI) uliofanyika Februari 9, mwaka huu jijini Arusha.


Kigahe, alisema nchi hizo zimekubaliana kusaidia sekta binafsi kukua kwa kuondoa vikwazo vya kibiashara, vikiwamo vya kikodi na kuboresha miundombinu katika maeneo ya mipaka ili kuimarisha sekta hiyo ambayo ina nafasi muhimu katika maendeleo ya uchumi wa EAC.

"Makubaliano mengine ni pamoja na kuhakikisha biashara zetu zinafanyika kwa haki sawa na ndio maana tuna Tume ya Ushindani (FCC) ambayo inahakikisha wafanyabiashara kutoka nchi za wenzetu wanafanya biashara kwa uhuru na kwa haki, pia tunahamasisha kuhusu ubora ndio maana tulikuwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa na kuuzwa EAC zinazingatia ubora," alisema Kigahe.

Alisema Tanzania inatarajia kuuza bidhaa zaidi nje ya nchi mwaka huu wa fedha wa 2024/2025 kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa katika sekta ya kilimo kutarajiwa kuongeza uzalishaji wa mazao, hivyo kuchochea mauzo ya nje. Mwenyekiti wa Mkutano huo na Waziri wa Biashara na Viwanda wa Sudan Kusini, William Anyuon Kuol, alisema pamoja na mambo mengine yaliyojadiliwa, sekta binafsi kuanzia zinatakiwa kupewa nguvu katika maeneo ya viwanda na uwekezaji.

Mkutano huo wa 43 pia ulizingatia tathimini ya kikanda kuhusu mafanikio ya eneo moja la forodha na ripoti ya hali ya utekelezaji wa mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia mizigo.

Maazimo ya mkutano huo yatawafikia wakuu wa nchi za EAC kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi.





# Wananchi: Tunakodishwa gari la kubeba wagonjwa

**Na Timothy Itembe,** MARA

BAADHI ya wakazi wa wilaya ya Tarime mkoani hapa, wameiomba serikali kuondoa utaratibu wa kukodisha gari la wagonjwa kutokana na kushindwa kumudu.

Wakazi hao, akiwemo Maria Joseph, walitoa ombi hilo juzi wakati wa hafla ya kukabidhiwa gari la wagonjwa lililotolewa na Serikali kwa Kituo cha Afya Magena.

Maria, alisema wanapokuwa na wagonjwa wanaohitaji huduma haraka, inawalazimu kukodi gari kulingana na umbali kuanzia Shilingi 150,000.

"Tunaipongeza serikali kwa kutupatia gari ambalo litakuwa suluhisho kwa wajawazito na wagonjwa wengine tunachoomba litusaidie na wasilikodishe," alisema Joseph.

Akikabidhi gari hilo lenye namba za usajili STM 7823, Mbunge wa Tarime Mjini, Michael Kembaki, alisema lengo ni kuboresha huduma katika sekta ya afya na kuondoa adha kwa wananchi ya kukosa usafiri wa kupeleka wagonjwa kwenye hospitali nyingine kwa ajili ya kunusuru maisha yao.

Kembaki, aliwataka viongozi na wasimamizi wa kituo hicho kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Tarime na Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo kuhakikisha wanafuatilia mwenendo wa gari hilo ili lifanye kazi iliyokusudiwa na Serikali.


Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Dk. Juma Musubi, alisema gari hilo litapunguza kero ya ukosefu wa usafiri kituoni hapo na kusaidia utoaji huduma bora za afya kwa wagonjwa.

Dk. Masubi, alisema kabla ya kukabidhiwa gari hilo, wagonjwa walikuwa wakiteseka kwa kukosa huduma hiyo kusafirishwa kwenda kupata matibabu katika Hospitali ya Bomani, Msoma na Bugando.

"Kwetu gari hii ni mkombozi katika utoaji huduma bora kwa jamii na awali tulipatiwa vifaa tiba zikiwemo mashine ya USD,ECG vitanda vya wagonjwa vya kisasa na kwa sasa tunakabiliwa na upungufu wa watumishi walioajiriwa," alisema Dk. Musubi

Alisema kituo hicho kina watumishi 23 na muuguzi mmoja wa kutoka Taasisi ya BMF.

Alisema kituo hicho kimeajiri watumishi wa mkataba 11 na kwamba kinakabiliwa na ukosefu wa jengo la kufulia nguo za wagonjwa na wodi.



Mwakilishi wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Benedict Mugambi (wapili kulia), akikabidhi ramani ya matokeo ya sensa ya watu na makazi ya wilaya ya Kishapu kwa Mkuu wa wilaya hiyo, Joseph Mkude baada ya kutoa elimu ya usambazaji na matumizi ya matokeo ya sensa hiyo ya mwaka 2022 kwa viongozi na makundi ya kijamii kwa ajili ya mipango ya maendeleo endelevu, wilayani humo mkoani Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mganga mkuu 'alilia' magari manne

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MGANGA Mkuu wa Manispaa ya Shinyanga, Dk. Elisha Robert amesema Manispaa hiyo inakabiliwa na uhaba wa magari manne ya wagonjwa na kusababisha kuzorota kwa huduma za dharura hususani kwa wajawazito kwa wakati.

Dk. Elisha alitoa kilio chake juzi wakati manispaa hiyo ikipokea gari la wagonjwa na vitanda kutoka kwa Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi.

Alisema katika manispaa hiyo uhitaji wa magari ya wagonjwa ni manne na kwamba kulikuwa na mawili, lakini moja liliharibika, hivyo kupata gari hilo imekuwa mkombozi kwa wagonjwa na kuomba juhudi zaidi kufanyika kuhakikisha wanapata magari ya kutosha.

Baadhi ya wakazi wa Manispaa ya Shinyanga, akiwamo Eliza Masanja, alisema upatikanaji wa magari ya wagonjwa ni muhimu hasa kwa wajawazito wanaohitaji kuwahishwa kupata huduma za kujifungua ili kuokoa maisha ya mama na mtoto.

Mbunge wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, akikabidhi gari hilo na vitanda, alisema hiyo ni sehemu ya ahadi zake katika kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

"Gari hili la wagonjwa ambalo nalikabidhi ni moja ya vitendea kazi muhimu katika sekta ya afya, kwa kubeba wagonjwa na kuwawahisha kupata huduma za matibabu na kuokoa maisha yao," alisema Katambi.

Alisema Serikali itahakikisha inaboresha upatikanaji wa huduma bora za afya, ikiwamo upatikanaji wa vifaa tiba, dawa na kukamilisha ujenzi wa zahanati.

Meya wa Manispaa hiyo, Elias Masumbuko, alisema wamefanyiwa maboresho makubwa na gari hilo lilipunguza uhitaji mkubwa uliokuwepo hospitalini hapo.

## KACU kutengeneza mafuta ya pamba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) mkoani Shinyanga kipo mbioni kuanzisha kiwanda cha kuchakata na kutengeneza mafuta ya kula ya mbegu za pamba ili kuinua uchumi wa wakulima.

Mpango huo ulitangazwa juzi na Mwenyekiti wa KACU, Tano Nsabi wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake kuhusiana na mikakati waliyopanga kwa kipindi cha mwaka huu.

Nsabi, alisema wameomba mkopo wa fedha Benki ya Kilimo (TADB) wa kuanzisha kiwanda cha kutengeneza mafuta ya kula yanayotokana na mbegu ya zao hilo.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuongeza mapato ya ndani kwenye ushirika na kulipa malipo ya pili wakulima, kuongeza uzalishaji na ajira kwa vijana.

Meneja wa Pamba KACU, Amir Mwinyimkuu, alisema chama hicho kimeleta ushindani wa bei ya ununuzi wa zao hilo na kampuni nyingine kwa kila msimu baada ya kuanza kununua na kuchakata, hivyo kuwasaidia wakulima kuinuka kiuchumi.

Alisema msimu wa kilimo wa 2019/20, chama hicho kilinunua zaidi ya kilo milioni 22, kati ya hizo, kilo 705, 571 kutoka wilayani Kahama, zaidi ya milioni 1.4 Kishapu, Nyang'hwale mkoani Geita kwa Shilingi 9,020 badala ya bei elekezi ya Shilingi 8,010 kwa kilo.

Mwinyimkuu, alisema ushindani wa bei wakati wa ununuzi wa pamba sokoni unawafanya wakulima kupata fedha ikilinganishwa na bei elekezi inayotolewa na Serikali.

Alisema msimu wa kilimo 2020/2021 walinunua zaidi ya kilo milioni 3.4 za pamba kwa Shilingi bilioni 5.5, wakati huo kilo moja ilinunuliwa kwa Shilingi 1,456 ikilinganishwa na bei elekezi ya Shilingi 1,200.

"Tulipandisha pia bei katika Msimu wa 2021/2022 kwa kununua kilo moja kwa shilingi 1,825 hadi 2,020 kwa baadhi ya maeneo, licha bei elekezi ya Serikali kuwa Sh.1,560, lakini kwa msimu wa 2022/2023 tumenunua kwa Shilingi 1,060 na ndio bei elekezi ya serikali," alisema Mwinyimkuu.

Mwenyekiti wa Chama cha Msingi Uyogo (AMCOS), Maganga Masanja, alitaja hatua ya ushindani ya KACU katika kununua pamba kwa bei kubwa imesaidia kurejesha faida kwa wakulima kama sehemu ya malipo ya pili.

Alisema chama hicho kina jumla ya wakulima 257 wanaolima zao hilo na msimu uliopita wa 2022/2023 walizalisha tani 50 za pamba na kuuza kwa bei elekezi iliyokuwa imepangwa na serikali 1060 na kwa KACU kununua pamba kulisababisha kuwepo kwa ushindani wa bei na kampuni nyingine.

ama
ALHAMISI FEBRUARI 15, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

## CWF na zawadi mafao aina yake, yamkonga waziri, aacha tabasamu



## MDOMONI MWA UMMY... Hatua inavyopiga katika vita VVU, Ukimwi, saratani safari inasuasua

Ukurasa 13

# Miaka mitatu ya urais na bidhaa mpya utalii afya ulionasa 2400

•Trilioni 67 zaokolewa; JKCI haina mpinzani EAC




Mratibu wa Utalii Tiba kutoka Wizara ya Afya, Dk. Asha Mahita, akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) Dk. Peter Kisenge, kitabu chenye Mpango Mkakati wa Utalii Tiba, kilichoandaliwa na Kamati ya Kitaifa ya Utalii Tiba, mwaka jana. **PICHA: MAKTABA.**

**Na Mwandishi Wetru**

NI miaka mitatu inaelekea katika kutimiza katika uongozi wa Rais Dk. Samia katika nafasi ya urais. Iko wazi tayari kuna mapinduzi makubwa katika ujenzi wa hospitali, zahanati na vituo vya afya, ikiwa sehemu ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM).

Wizara ya Afya, Disemba mwaka jana ikatenga shilingi trilioni 6.7, katika uongozi wa Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, ikijumuisha maboresho kitalamu na kiteknolojia, Lengo ni wananchi wengi waweze kupata matibabu ya kibingwa ya magonjwa mbalimbali yakiwemo ya moyo.

Naibu Waziri wa Afya Dk. Godwin Mollel anatumia mfano wa huduma kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), inayovyosambaza teknolijia na ujuzi wake wa kibingwa mikoani.

Hiyo inakuja huku, Februari mwaka huu, na Makamu wa Rais Tanzania Dk. Philip Isdor Mpango ametamka ushindi katika sekta ya afya

Hapo anaoroshesha wagonjwa wa moyo zaidi ya 800 wamefanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo huku wengine zaidi ya 2,000 kufanyiwa upasuaji wa tundu dogo kwa kutumia mtambo wa 'cathlab' kwa kipindi cha miaka Miwili katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI).

Hapo anaeleza zao jingine la Serikali Awamu ya Sita, Utalii Tiba wageni 2,400 wakimiminika kutoka nchi waliotoka nchi za jirani za Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya DRC, Kenya, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Uganda na Zambia.

Anasema, kutokana na huduma zinazotolewa na Taasisi hiyo zimeweza kuifanya JKCI kuwa taasisi ya umma inayoongoza katika kutoa huduma za matibabu ya moyo Afrika Mashariki na kati, hivyo kuwavutia wanataaluma kutoka nchi za jirani zikiwemo nchi za Malawi, Zambia na Rwanda kujenga mashirikiano.

Mchumi Dk. Mpango, anasema kupitia Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, serikali imeokoa shilingi bilioni 63 ambazo zingetumika kwa ajili ya matibabu ya moyo nje ya nchi.

"Kati ya mafanikio yaliyofanywa na taasisi hiyo ni pamoja na uanzishwaji wa kambi maalumu ya matibabu ya moyo ijulikanayo kwa jina la 'Dk. Samia Suluhu Hassan Services' ambayo imekuwa ikitoa huduma ya kuwajengea uwezo wataalamu wa Afya walioopo katika hospitali za mikoa na kuwafikishia karibu huduma za matibabu ya moyo wananchi wanaohitaji matibabu hayo," anasema Dkt. Mpango

Pia amesema, serikali itaendelea kuwekeza kakika taasisi hiyo kwa kupanua huduma za matibabu na kumtaka Waziri wa Afya Ummy Mwalimu ameagizwa kufuatilia gharama za ujenzi utakaofanyika Dar es Salaam, mapema ili serikali iwekeza katika ujenzi huo.

Hadi sasa, JKCI, imekuwa katika mkakati wa kuanda mkutano wa kujumuikia kisayansi kwa wataalamu wa afya nchini, lengo ni kuwapa ujuzi wataalamu kuhusu magonjwa ya moyo.

**KUTOKA WIZARA AFYA**

Dk. Molle JKCI katika mikoa tofauti nchini wanaweka kambi ya kitabibu, ikifanyika bila ya malipo yoyote, serikali inagharamia na kwa JKCI hufanya mara nyingi, akishukuru ni zao la Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

Pia katika tiba mkoani wanatoa nafasi kwa wale wanaokutwa na matatizo ya moyo kupata rufani ya kutibiwa mapema kwa kupewa rufaa na kuwajengea uwezo wataalamu wa hospitali husika ili baada ya kumalizika kwa kambi ya matibabu nao waweze kuwatambua na kuwatibu wagonjwa wa moyo.

AFYA

# CWF na zawadi mafao aina yake, yamkonga waziri, aacha tabasamu

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (CWF), umekuwa 'ukiwafuta machozi' wafanyakazi wanaopatwa na majanga na kufa wakiwa kazini, wao na wanufaika, huku wakitoa ushuhuda 'ni mfuko wa maajabu.'

Nchini CWT inabeba jukumu la kuwavuta karibu wanachama wake wanufaika, kwa kuwapa matumaini ya kuendelea kuishi kwa mafao yao, ili wajikimu na maisha ya kila siku.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Profesa Joyce Ndalichako, kufika katika Ofisi za CWF akiwa katika makao makuu ya CWF, Dar es Salaam, ikiwa sehemu ya Maadhimisho ya Kimataifa ya Siku ya Watu Wenye Ulemavu Duniani iliyofanyika Desemba mwaka jana mkoani Dodoma, ana maoni yake.

Akitokea mkoani Ruvuma kwa ziara ya kikazi kukagua ujenzi wa Chuo cha Walemavu Songea, akaamua moja kwa moja kufika kwenye ofisi za CWF, shauku anaitaja ni kukutana na wanufaika hao.

Miongoni mwao walikuwamo watu waliopata ulemavu kazini, wajane wawili, mmoja aliyekuwa mfanyakazi wa Benki Tanzania (BoT) na wa Wizara ya Viwanda na Biashara na watoto wao ambao ni sehemu ya wanufaika wa mfuko huo.

Kabla ya wanufaika hao kuanza kuelezea walichokifananisha na maajabu ya mfuko huo, Profesa Ndalichako akanena: "Nimeona hapa lazima nije kuonana nanyi, ikiwa sehemu ya Maadhimisho ya Kimataifa ya Siku ya Watu Wenye Ulemavu Duniani.



Mkurugenzi wa Huduma za Tathmini wa CWF, DK.Abdulsalaam Omar, akiwa na mnufaika wake, Deus Anthony, mjini Morogoro mwaka jana. **PICHA: MTANDAO.**

"Niliposhuka kwenye ndege (Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam) kutoka Songea nimekuja moja kwa moja hapa, tuzungumze," anasema huku akiwa ni mwenye tabasamu.

Mkuu wa Idara katika CWF, Dk. Abdulsalaam Omar, anawatambulisha wanufaika hao kwa Waziri Ndalichako kuwa wako saba, akiwataja kwa majina; Joseph Joseph, Emacullate Igula, Michael Asenga, Veronica Magaya, Robert Tesha na Kelvin Cameroon.

Cameroon, anasema alikumbwa na mkasa wa kujeruhiwa mguu wake wakati akitoa tope la saruji, lilikokuwa limeganda kwenye gari la kuchanganyia bidhaa hiyo na malighafi nyingine.

Cameroon anasema, aliajiriwa kwenye kampuni hiyo ya ujenzi iliyopo Tegeta, Dar es Salaam kwa nafasi fundi bomba na kwamba na wenzake walikuwa wakiingia kwa zamu kwenda kusafisha magari hayo, yalikuwa na mitungi inayozunguka kwa ajili ya kuchanganya saruji, mchanga na kokoto.

Anasema katika kuhakikisha saruji hiyo inatoka, walilazimika kutumia nyundo kugonga kwa nguvu badala yake ilimpiga kwenye mguu wake wa kushoto na kumvunja nyonga.

Mnufaika huyo anasimulia baada ya kushauriwa na daktari aliyekuwa akimtibu katika hospitali iliyopo Tegeta, Dar es Salaam, kwa gharama za mfuko huo, akaenda katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa matibabu zaidi na kufika Februari mwaka jana, alifanyiwa upasuaji na kuanza kutembea kwa kutumia magongo.

Cameroon na wanufaika wengine saba, sasa wanawapongeza waajiri wao kwa kuchangia kwenye mfuko huo na kuwawezesha kupata matibabu na mafao.

Vilevile yeye na wenzake, wanaushukuru mfuko huo, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na Waziri Ndalichako, kwa kuwaondolea hali ngumu ya maisha wao na wategemezi wao.

Awali, Pofesa Ndalichako akawafariji wafanyakazi waliopata ulemavu wakiwa kazini wanaopatiwa mafao na CWF katika ofisi za mfuko huo jijini Dar es Salaam, wake kuwasihi waendelee kuwahudumia waume zao waliopata ulemavu.

**MAFAO MAPYA**

Anatumia fursa hiyo kuwa serikali imeongeza fao jingine la 'Huduma za Utengemao kwa Wafanyakazi Waliopata Ulemavu Wakiwa Kazini.'

"Hivi karibuni tutaanza kutoa huduma ya utengamao kutegemea na mwathirika mwenyewe atakavyotaka kutegemea na ulemavu," anasema.

Waziri anaendelea: "Tutakuwa tunampeleka kwa gharama za mfuko kwenye mafunzo... tutatoa huduma kukabiliana na mazingira kwa mfano vyoo anavyotumia, kubadilisha mazingira ya nyumbani."

Waziri Ndalichako anasema kuwa, serikali inatambua umuhimu wa mifuko inayowezesha wafanyakazi na kupitia WCF inatarajia kuanzisha fao jipya la huduma ya mtengamao.

Anasema, ni Mafao yanayotarajiwa kuanzisha Elimu ya Ufundi Stadi kwa Wafanyakazi Waliopata Ulemavu Kazini, ikisaidia kubadilisha mazingira ya nyumba kulingana na ulemavu waliopata.

Profesa Ndalichako anasema, imewekewa riba rafiki, kutoka asilimia 10 mpaka asilimia mbili kwa mwezi, ili kuwapo mazingira wezeshi kwa wawekezaji.

"Naomba kuhamasisha waajiri kuweza kuwachangia wafanyakazi wao, kwani viwango vya uchangiaji ni vidogo," anatamka mnufaika Nobert Tesha, anayesema serikali imepunguza viwango vya uchangiaji hadi kufikia asilimia 0.5.

Mnufaika mwingine aliyejitambulisha kuwa 'Mchungaji' anafafanua kwamba yeye na watoto wake wanne wananufaika, akisema": Nilipoanza kupata ile fidia kutoka WCF haijawahi kuchelewa. Ikifika tarehe, kuna meseji inaingia kwenye simu yangu..."

Anasema kuna wakati alikuwa akijiuliza "anawezaje kupata nafasi ya kusema kuhusu WCF."

Naye Kelvin Cameroon anasema: "Mheshimiwa Waziri napenda kushukuru sana uongozi wa mama Samia Suluhu Hassan pamoja na wewe. Naweza kusema endelea na matibabu, napenda kushukuru taasisi ya WCF na naomba iendelee na moyo huo muweze kusaidia watu zaidi."

Lengo la mfuko wa fidia kwa wafanyakazi, linatajwa ni kumrejesha mfanyakazi anayeumia katika hali yake ya kawaida kipaumbele namba moja na kwa sababu hiyo.

Mfanyakazi anapoumia kazini, ananuika na matibabu katika hospitali anayoichagua, Waziri Ndalichako akisema, pia mwanachama na wategemezi wake wanapata matibabu kulingana na kiasi cha fedha walichochangia, lakini CWF hauna ukomo.

"Mfuko huu hauna ukomo wa kumlinda mfanyakazi, lengo letu ni kulinda rasilimali, mfanyakazi ameumia kazini, ili mwisho wa siku aweze kurejea kazini na katika hali yake," anasema.

Waziri huyo anasema, pia mfuko huo unatoa fidia ya ulemavu wa muda na wa kudumu na kwamba, hivi karibuni wataanza kutoa mafao ya huduma ya utengamao.

"Hii huduma ya utengamao tutaanza kutoa mafunzo ya kujenga ujuzi kwa wafanyakazi wanaopata ulemavu wakiwa kazini," anasema.

Anasema aina ya ufundi watakayotoa inalingana na hitaji la mfanyakazi, ili kumpa ujuzi utakaoendana na ulemavu wake.

"Unaweza kukuta mtu alikuwa anategemea kufanya kazi kwa kutumia miguu yake kwa bahati mbaya miguu imekatika kwa hiyo yeye anaweza akabadili kazi sasa na mikono ikaweza kutumika. Kwa hiyo katika kusomea kwake anaweza akasomea kutumia mikono," anasema Ndalichako.

Kwa mujibu wa Profesa Ndalichako, wataanza kutoa huduma kwa kumpeleka kwa gharama za mfuko kwenye mafunzo kupata ujuzi mpya, ambao anaona utamsaidia kujiajiri na kumrudisha nyumbani kwake.

Kimsingi, utakuwa unatoa huduma ya kumwezesha mgonjwa kukabiliana na mazingira, ikiwamo aina ya vyoo anavyohitaji mhusika, pia kuwapo mafao ya kubadilisha mazingira ya nyumbani kwa mnufaika.

**MAGEUZI KIUFUNDI**

Ikirejewa takwimu za CWF, madaktari wenye ujuzi kufanya tathmini ya ulemavu unaotokana na ajali na magonjwa wamefikia 1,722 nchi nzima, mradi ulioanza miaka minane iliyopita, kwa kutoa mafunzo kwa madaktari husika.

Baadhi ya mambo ambayo madaktari hao wamejifunza ni Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi; Mchakato wa Uwasilishaji Madai; Dhana ya Usalama na Afya Kazini na Jinsi ya Kudhibiti Vihatarishi kazini.

Mengine yanatajwa ni; tathmini ya vihatarishi, kuchunguza magonjwa yatokanayo na kazi; Udhibiti wa Ajali na Magonjwa Kazini; Kufanya Tathmini ya Ulemavu; Tathmini ya Magonjwa yanayoendana na mfuko, kijamii na kiuchumi.

Pia, kuna majanga yatokanayo na kazi, familia zao na waajiri kwa kutoa fidia stahiki kwa usawa, uendelevu na ufanisi.

CWF imekuwa ikitoa matibabu kwa wafanyakazi waliougua na kujeruhiwa kazini hospitalini, kuweka viungo bandia na mafao kama hawataweza kurudi tena kazini.

Vilevile imekuwa ina mafao kwa wategemezi endapo mfanyakazi atafariki dunia, kusomesha watoto hadi wanapofikia umri wa miaka 18 ambao kisheria wanatambulika kuwa ni watu wazima.

Mahakama Kuu Tanzania Divisheni ya Kazi imetangaza kushirikiana na WCF wa kuzifanyia marekebisho baadhi ya sheria kuhusu ulipaji wa fidia ili kuboresha huduma za fidia kwa walenga kwa manufaa ya Watanzania.

AFYA

## KUTOKA MDOMONI MWA WAZIRI UMMY…

# Hatua inayopigwa katika vita VVU, Ukimwi; saratani safari inasuasua

**Na Yasmine Protace**

KATIKA mapambano ngazi duniani kukabili maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), Tanzania imo katika rekodi bora kudhibiti maambukizi hayaongezeki kwa jamii.

Ni hatua inayoendana na tiba, pia elimu kupambana na maambukizi hayo, wagonjwa wakihimizwa kutumia dawa kwa wakati, vilevile wanajilinda dhidi ya ngono zembe, kuwaepushua na maambukizi mapya ya VVU.

Hapo wagonjwa wanahudhuria kliniki na kupatiwa elimu ya matumizi sahihi ya dawa, mahudhurio ya kliniki kwa wakati, hali ambayo kitaalamu inasaidia kumlinda mgonjwa na maambukizi mapya.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema maambukizi ya VVU nchini yamepungua kutoka asilimia saba mwaka 2003/2004, hadi asilimia 4.4 mwaka 2022/2023, kukiwapo tofauti kati ya watu na maeneo mbalimbali ya kijiografia.

Ni matamshi yake Waziri Ummy, akiwa Dar es Salaam anapofungua Mkutano wa Siku Mbili wa Mapitio ya Kimkakati uitwao Pepfar CoP Muhula wa 23, lengo ni kutathmini hatua iliyofikiwa kuhusu mwitikio wa VVU na Ukimwi kudhibitiwa ifikapo mwaka 2030.

"Kikao hiki kinalenga kujadili na kubainisha mikakati itakayowezesha ufanisi wakati wa utekelezaji wa afya za msingi na kubainisha ufanisi utakaowezesha kufikia malengo kabambe yaliyoainishwa katika sera na nyaraka za kimkakati za nchi," anasema.



Moja ya kampeni za kupima virusi vya Ukimwi, ilipokuwa mkoani Dodoma. **PICHA: MAKTABA**

Pia anaongeza, kuwapo kipaumbele katika masuala ya VVU na Ukimwi ni pamoja na kulinda mafanikio yaliyofanyika, kupunguza maambukizi mapya hususan kwa vijana balehe, kama ilivyo kuondoa kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Ummy anasema, Tanzania imepiga hatua kubwa katika nyanja mbalimbali za VVU, akirejewa ripoti ya Mpango wa Umoja wa Mataifa Unaoshughulika na Ukimwi (UNAIDS 2022), kwamba imeufikia Mkakati wa Kimataifa wa Ukimwi 2021 hadi 2026 katika matibabu.

"Mafanikio hayo yamechangiwa na matokeo ya Utafiti wa Athari za VVU Tanzania Mwaka 2022-2023 (HIV 2022-2023) ambao uliripoti kufikiwa kwa malengo ya UNAIDS 95-95-95 kwa 82.7%, 97.9% na 94.3% (ngazi ya jamii)," anasema. Anaongeza kuwa asilimia 95 ya wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU, wanafahamu hali zao za VVU; pia asilimia kama hizo wanatumia dawa za kufubaza VVU wanaotumia ARV, wamefikia hali ya kufubaza VVU.

Waziri Ummy anatumia fursa hiyo kuwashukuru washirika kimataifa; Pefpar, Global Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Watoto (UNICEF), Asasi ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo (USAID), CDC, DOD pamoja na Kikosi Maalum cha Amani cha Marekani (Peace Corps).

Anataja nyenzo hizo zote zimekuwa na msaada wa usioyumba wa kiufundi na kifedha kwa serikali nchini, kukabili na kudidimiza janga la VVU na Ukimwi, ifikapo mwaka 2030.

### NAFASI YA SARATANI

Kuhusu ugonjwa wa saratani, Waziri Ummy, anaanza ana tahadhari kwamba, iwapo jamii isipochukua hatua stahiki, vifo vya saratani vitaongezeka maradufu, kila mwaka inaguisa wagonjwa wa 40,000 na kupatikana vifo 26,000.

Waziri anafafanua, wagonjwa wanaofika hospitalini wako ni asilimia 30 pekee, wengi wanabaki mitaani wakishindwa kufika katika vituo vya kutoa huduma za afya.

Pia, anasema kupitia mradi huo ulioanzishwa kwa huduma za saratani nchini, kutasaidia kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi na muda wa matibabu yao.

"Nikiangalia takwimu zetu kwa mwaka 2021/22, wagonjwa 89 walipelekwa nje ya nchi. Tumetumia kiasi cha shilingi bilioni 4.8 na kwa wagonjwa wa saratani pekee, imetumika shilingi bilioni 3.1 (65%).

"Pia kufuatia kituo hiki, tutaongeza huduma za tiba utalii (wagonjwa kutoka nje kuja kutibiwa Tanzania)," anafafanua Waziri Ummy.

Pia anasema zaidi ya asilimia 80 ya wagonjwa wa saratani wanaofika hospitalini, hali zao zinakua katika hatua ya tatu hadi ya nne, ambayo inachangia kuwapo ugumu wa matibabu, tofauti na ambavyo angewahi kujua hali yake na kuanza matibabu mapema.

"Nitoe wito kwa Watanzania wapime saratani angalau mara moja kwa mwaka kwa kuwa saratani inayoongoza ni ya mlango wa kizazi kwa asilimia 25, matiti asilimia 10, tezi dume asilimia 9, mfumo wa chakula asilimia 6.5 na saratani nyinginezo." anasema.

Katika hatuia ya tahadhari, Waziri Ummy anasema suala la saratani nchini linahitaji uwekezaji, hapo akitaja dira ya kutanua wigo wa kudhibiti na kuwahimiza watu kupata huduma mapema.

Waziri anajumuisha pia mustakabali wa magonjwa yasiyoambukiza, kwamba Watanzania wanapaswa kufuata mtindo bora wa maisha, ili waepuke magonjwa yasiyo ya kuambukizwa.

Anataja kuzingatia mtindo bora wa maisha unaoepuka magonjwa yasiyoambukiza, kwa kuwa takwimu za mwaka 2012, zinaonyesha Watanzania tisa kati ya 100 wana kisukari, huku 26 kati ya 100 wana shinikizo la juu la damu.

Waziri anatamka hayo kwenye ufunguzi wa Kongamano la Kimataifa litwalo 'Heart Team Africa' lililofunguliwa na Makamu wa Rais wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, mjini Zanzibar.

"Kulingana na Utafiti wa Step WHO za mwaka 2012 (tunaposubiri data za 2022 kutolewa hivi karibuni), zinaonyesha Watanzania tisa kati ya 100 wana kisukari, huku Watanzania 26 kati ya 100 wana shinikizo la juu la damu," anasema Waziri Ummy.

Anataja vitu vya kuzingatia ni pamoja na kupunguza matumizi ya sukari, chumvi, mafuta, kuacha matumizi ya tumbaku, unywaji pombe uliopitiliza, kuongeza kasi ya mazoezi ya kila mara, ikiwamo mazoezi ya viungo.

Waziri anasema, serikali itaendelea kuwekeza kwa kuboresha matibabu ya moyo nchini na upande wa majengo, kuwa na vifaa tiba vya kisasa vinavyofanana, vilivyopo katika nchi zilizoendelea, pamoja na kuwaendeleza wataalamu wa moyo kuwa mabingwa waliobobea.

"Serikali imetupa fedha kiasi cha shilingi bilioni 9 kwa ajili ya kusomesha madaktari kuwa mabingwa wabobezi katika masuala ya moyo na hii itahusisha wataalamu wa afya ambao ni madaktari wa upasuaji, wauguzi, wafamasia na madaktari wa usingizi," anasema Waziri Ummy.

Anasema, serikali nchini imefanikiwa sana, hivyo inaendelea na kuokoa maisha ya Watanzania wenye magonjwa yasiyoambukiza, ikiwamo kutoa matibabu na elimu.

"Tunaona fahari kubwa kwa yote ambayo tumefanikiwa katika vituo vyetu vya huduma za afya ikiwamo kutoa huduma ya hali ya juu nchini Tanzania," anatamka, akiwa na mifano:

"Kama vile upandikizaji wa valvu ya mishipa, kwenye Taasisi ya JKCI (Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete), upasuaji wa 'Transcatheter' kwa kutumia Angio Suite katika Taasisi yetu ya Kitaifa ya Mifupa (MOI)."

Waziri Ummy anasema, mkutano huo umeangaziwa mada mbalimbali za kujadiliwa hapo, ikijumuisha namna ya kuchunguza upigaji picha; upasuaji wa mishipa; urekebishaji viungo; uuguzi na kinga, ambao majadiliano hayo muhimu yantarajiwa kubadilishana uzoefu kati ya wajumbe wote waliokusanyika.

AFYA

## SIKU YA KIFAFA DUNIANI

# Mgonjwa na madhila, unyanyapaa; profesa bingwa na undani kitaalamu

**Na Mary Geofrey**

KIFAFA ni ugonjwa sugu wa neva ambapo ubongo hufanya kazi kwa njia isiyo ya kawaida na husababisha mshtuko wa mara kwa mara.

Aidha, kifafa ni dalili za matatizo ya ubongo ambayo yanaweza kutokea ghafla na kusababisha shughuli ya umeme isiyo ya kawaida katika ubongo, kupoteza fahamu, na degedege kwa muda mrefu (mwili hutetemeka bila kudhibitiwa). Inaweza kuathiri watu wa rika zote, bila kujali jinsia zao, rangi.

Licha ya ugonjwa huo kutambulika na wataalamu wa afya duniani kote, bado imani potofu kuhusu ugonjwa huu ni tatizo sugu linalosababisha watu wengi kupoteza maisha.

Aidha, zaidi ya jitihada zinazofanywa na Wizara ya Afya, kutoa tiba sahihi za ugonjwa wa kifafa katika vituo vyote vya afya nchini, bado uelewa mdogo ni tatizo linalokwamisha juhudi hizi za serikali.

Katika kuadhimisha Siku ya Ugonjwa wa Kifafa Duniani kila Februari 13, Nipashei inaangazia wagonjwa wa kifafa, wazazi na wataalamu wa afya kuhusu madhila wanayopitia na namna jamii inaweza kubadili mtizamo wake kutoka kwenye imani za kishirikina na kuamini ni tatizo la kitaalam na linalotibika.

Kwa mujibu wa wataalam wa afya, imani potofu kuhusu ugonjwa wa kifafa ndio sababu kuu ya wagonjwa wengi wenye tatizo hilo kutegemea tiba mbadala kama nyumba za ibada, waganga wa kienyeji, wapiga ramli na kupuuza tiba za hospitali.

Wagonjwa wa kifafa wanapoteza maisha kwa kudondoka katika mazingira hatarishi yenye vitu vya ncha kali, maji au moto.

**SIMULIZI YA MGONJWA**

Omari Vadega (25) ni kijana aliyegua kifafa kwa miaka 12, ugonjwa ulimuanza gafla akiwa na miaka 13, akifafanua: "Nilikuwa mzima wa afya tele, nikiwa na miaka 13 ndipo nilianza kudondoka kifafa."

Anasema licha ya kuanza kuuguma ugonjwa huo akiwa na miaka 13 baada ya kuzunguka kutafuta tiba mbadala, alianza matibabu ya hospitali akiwa na miaka 21 na kufanikiwa kukata minyororo ya kunyanyapaliwa, umasikini na kuwa balozi wa kusaidia wengine kupatiwa matibabu.

Anasema tangu aanze kupatiwa matibabu hajaanguka kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa, kutoka kuanguka mara tatu kwa siku hii ni kwasababu amezingatia matibabu na matumizi sahihi ya dawa.

Omari anasema kwanza alifanikiwa kuvifahamu vichocheo vinavyomfanya aanguke kifafa ili kuwahi kuchukua tahadhari na hivyo kumpunguzia madhara kama majeraha na kudhalilika.

"Kabla sijaacha kudondoka, nilipata matibabu nikafuata masharti. lakini nikafahamu vichocheo vinavyoashiria kuanza kudondoka ambavyo mwanzo sikuwa navifahamu. Hivyo, nilipokuwa nahisi kudondoka nilikuwa naomba msaada wa haraka kwa wale niliona jirani lakini hata kujiandaa mwenyewe ili nisidhalilike," anasema Omari.

Omari ambaye sasa ni Balozi wa kuelimisha wagonjwa wengine wa kifafa, anasema tatizo kubwa linalofanya wagonjwa wa kifafa kudondoka ni kukosa tiba mapema lakini pia kutofahamu vichocheo au dalili za kuanza kudondoka.

Anasema, kwa sasa hajadondoka kwa muda mrefu kwasababu anatumia dawa, anafuata masharti anayopewa na wataalam wa afya.

"Bado tatizo kubwa ni uelewa wagonjwa wengi wamekata tamaa kwa sababu ya imani walizomezeshwa kutoka kwa watu wanaowazunguka, bibi na babu hawaamini katika matibabu ya hospitali," anasema.

**UNYANYAPAA KABLA**

Kabla ya kuanza matibabu kwa miaka nane, Omari alidhalilishwa na kunyanyapaliwa na watu wake wa karibu kuanzia familia yake, majirani hadi shuleni, ambako walikuwa hawampi kipaumbele masomoni wala michezo kwasababu waliamini ni mtu wa kudondoka muda wowote.

"Kuna siku nilianguka kwenye daladala, nikapata msaada kutoka kwa mdogo wangu wakanirudisha nyumbani, nilipozinduka nikabadli shati kwasababu lilichafuka sana, nikavaa tisheti la shule.

"Niilipofika shule nikiwa mstarini nyuma kabisa, alikuja mwalimu akanikata mtama kwa sababu nimevaa shati chafu bila ya kunipa muda wa kujieleza, ilihali wanafahamu nina tatizo la kifafa.

"Huo ulikuwa mwanzo wangu wa kuchukia shule na kutamani kukaa nyumbani kwa sababu, nilijiona sistahili tena kuchangamana na wengine, wala sina nafasi ya kusikilizwa," anasimulia Omari.

Anasema aliacha kwenda shule lakini nyumbani nako wakaanza kusumbua kwa sababu alikuwa mzigo hawezi kufanya kazi yoyote kuhofia kundoka.

"Namshukuru Mungu baada ya matibabu niliweza kuanza kujitafuta, nikasomea mambo ya IT na sasa nafanya kazi, nimeanza pia lengo ni kuwaelimisha waende hospitali ndiko kwenye matibabu sahihi," anasisitiza.

Anasema tayari amesaidia vijana 17 kufahamu vichocheo vyao kabla ya kufikia hatua ya kuanguka na wanaendelea na matibabu katika maeneo mbalimbali nchini.

**CHANGAMOTO ZAKE**

Omari anasema wagonjwa wengi wanaougua ugonjwa huo hawana kazi za kufanya, wametengwa hivyo anapowafikia kuwasaidia wanategemea kupata msaada wa kazi au fedha na siyo matibabu.

"Mimi mwenyewe sina uwezo wa kuwasaidia natamani kwanza niwaondolee hili tatizo la kuanguka kwa kuwashauri na kuwapa maelekezo ambayo mimi nilipewa na nimepona naweza kuendelea na kazi zangu," anasema.

Anashauri, serikali inatakiwa kuweka nguvu zaidi ya kifedha na matibabu kwa kundi hilo la watu wenye matatizo hayo ili kuwasaidia kufahamu kwanza ndipo wakubali kutibiwa.

Pia, anasema, nafasi ya serikali kusogeza huduma karibu zaidi, kutoa dawa za kutosha na bure ili wanaougua iwe rahisi kufika hospitali kupata matibabu.

**KISA CHA MZAZI**

Mzazi wa mtoto wa miaka saba mwenye tatizo la kifafa kikali, Fides Uiso, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Tanzania Epilepsy Organisation, anasema unyanyapaa ni tatizo kubwa kuliko ugonjwa wenyewe kwasababu jamii inakuwa na imani potofu zinazokinzana na matibabu ya hospitali.

Anasema, alichelewa kumpatia matibabu mtoto wake kwa kile alichokua akimini ni imani potofu. Alipomwanzishia matibabu hospitali, sasa ameanza hatua ya kutembea na kuanza kuzungumza maneno machache.

"Sasa nimekuwa balozi nina shirika linalosaidia wazazi na watoto wenye tatizo hili kwanza kabisa kuwapa elimu ya namna ya kutibu ugonjwa huu na kuwahimiza kuwahi hospitali," anasema Fides.

Anashauri serikali inatakiwa kuendelea kuelimisha jamii kuhusu tatizo hili siyo imani za kishirikina bali na ugonjwa kama yalivyo mengine.

**CHANZO CHA TATIZO**

Profesa wa Magonjwa ya Mishipa ya Fahamu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, William Matuja, Prof. William Matuja, akizungumza kuhusu Maadhimisho ya Kumbikizi ya Siku ya Watu wenye Ugonjwa wa Kifafa, anasema unyanyapaa, udhalilishaji na upweke ni sababu inawafanya wagonjwa wenye tatizo la kifafa kuendelea kubaki nyumbani badala ya kwenda hospitali.

Anataja sababu za ugonjwa huo ni matatizo ya uzazi mama kupata shida wakati wa kujifungua, ugonjwa wa degedege unaojirudia kwa watoto wadogo, homa ya malaria kupanda kichwani na kusababisha kifafa.

Prof. Matuja ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Wataalam wa Kifafa nchini, anasema mgonjwa anaweza kupona na kuepuka majeraha ya ajali za kudondoka endapo atawahi matibabu ya hospitali.

**MSIMAMO WA SERIKALI**

Akizungumza wakati wa maadhimisho hayo, Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, anasema mpango wa serikali ni kuwafikia wagonjwa wengi kwa njia ya elimu ili wapate huduma za matibabu sahihi ya hospitali ambayo yanapatika katika hospitali zote za umma kuanzia ngazi ya jamii.

Anasema takwimu zinaonyesha duniani watu milioni 50 wanaugua ugonjwa huo wakati nchini kuna watu kati ya 20 hadi 30 kati ya watu 1,000 na tatizo kubwa linalofanya wengi kukosa matibabu sahihi ni wengi kuendelea kuwa na imani za kishirikina.

Anasema lengo la maadhimisho hayo duniani ni kuendelea kuelimisha jamii kuhusu ugonjwa huo ili watu wajitokeze kupata matibabu kaunzia kwenye vituo vya afya.

Prof. Tumaini anasema serikali inaendelea kuongeza vituo vya kutoa huduma ili wote wenye shida wapate matibabu haraka na kupona kabisa.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), ugonjwa wa kifafa huathiri watu milioni 50 duniani kote na asilimia 80 wakiwa katika nchi zinazoendelea. Hata hivyo asilimia 75 ya watu hao hukosa matibabu ya ugonjwa huu.




Profesa wa Magonjwa ya Mishipa ya Fahamu na Mwenyekiti wa Chama cha Kifafa Tanzania, William Matuja, akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ugonjwa wa Kifafa, katika Hospitali ya Mloganzila, Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA.**



# Waandishi wafundwa uchaguzi wa mitaa

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAMILIKI wa vyombo vya habari na waandishi wa habari wametakiwa kutoa nafasi kwa vyama vya siasa ili uchaguzi uwe huru wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika nchini mwaka huu uwe huru wa haki.

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mathew Kundo alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua Mkutano wa Mwaka wa Vyombo vya Utangazaji nchini sambamba na kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Utangazaji Duniani, ulioandaliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Kundo, alisema vyombo vya habari vina nafasi kubwa katika kipindi hicho hivyo ni vyema kuzielewa kanuni watakazojadili katika mkutano huo ili kuwa na uelewa wa pamoja wa namna bora ya kufikisha ujumbe kwa jamii. "Katika kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa vyombo vya habari vinatakiwa kuwa mstari wa mbele kuzingatia maadili na kanuni za utoaji habari kwa jamii kwa maslahi ya taifa kwani vina wajibu mkubwa katika taifa letu, hivyo ni muhimu kila mmoja kuzingatia taaluma na kutimiza majukumu yake kwa weledi," alisema Kundo.

Alivitaka vyombo vya habari kuanzisha vipindi vya kuhamasisha mila na desturi ya Mtanzania ili kuwaelimisha vijana kuhusu tamaduni zao.

"Ni muhimu sana kwenu TCRA kuliangalia suala hili kwa umakini mkubwa kwani mkifanya hivi itawasaidia sana kufanya kazi kwa ufanisi na sisi kama Serikali tunawaahidi kuendeleza ushirikiano uliopo ili kuleta maendeleo kwa jamii, " alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TCRA, Jones Kilimbe, aliwataka watangazaji na waandishi wa habari kuzingatia madili na kanuni ya kazi zao.

Alisema TCRA kama wadau wa utangazaji watahakikisha wanakuwa bega kwa bega na vyombo vya utangazaji kuhakikisha wanatoa mwelekeo wa maudhui yenye ubora bila upotoshaji.

" Maudhui ya utangazaji ni chakula kwa jamii, yanaweza kujenga au kubomoa, kuharakisha maendeleo au kukwamisha, hivyo ni jukumu la vyombo vya utangazaji kujikita katika kuhabarisha umma maeneo yenye tija na kuachana na uchochezi au uvunjifu wa madili," alisema

Mwenyekiti wa Wamiliki wa Vyombo vya Habari nchini (MOAT), Samwel Nyala, alisema pamoja na kukuza tasnia ya habari nchini bado kuna changamoto mbalimbali ikiwemo gharama kubwa ya leseni hali inayowakwamisha na kuwapa hasara ya uendeshaji .

Mdau wa habari kutoka Chama cha Watangazaji (NIBA), Amos Ngosha alieleza masikitiko yake kuhusu hali ya uchumi wa vyombo vya habari kuwa imedorora kwa kukosa ruzuku kutoka serikalini.

Aliiomba Serikali kuanza kutoa ruzuku kwa vyombo vya habari ili viweze kujiendesha.

"Tunashindwa kujiendesha kwa kukosa matangazo, matangazo yetu yamekuwa ni ya waganga wa tiba asili na viongozi wa dini, tunatozwa kodi kubwa kuliko faida tunayoipata, " alisema na kuongeza:

"Tunaomba taaluma hii iheshimiwe kwa kutupunguzia gharama za uendeshaji tuache kuwategema watu wa tiba mbadala katika uchumi."

## Wanaokiuka maadili ya afya kibano chaja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema haitasita kuwachukulia hatua wataalam wa sekta ya afya wanaokiuka maadili ya utumishi na kuwafutia leseni.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange alitoa kauli hiyo juzi wakati akifungua mkutano wa waganga wafawidhi wa vituo vya afya ngazi ya msingi wa kujadili utekelezaji, mafanikio, changamoto na fursa katika utoaji wa huduma bora za afya, ustawi wa jamii na lishe kwa wananchi.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri Mohamed Mchengerwa alisema kuwa: "Wataalamu afya wanapaswa kujua kuwa kazi yao zinahusisha maisha ya watu na zinaweka mzigo mkubwa wa dhamana na kuwa kutokana na umuhimu huu Serikali haitasita kuchukua hatua kwa watumishi wazembe."

Alisema wameanza kuchukua hatua kwa baadhi watumishi kwa kuwafutia leseni baada ya kuthibitika kwa uzembe, kukiuka sheria na kanuni za kazi zao, hivyo hawatafanya kazi yoyote ya afya nchini.

"Waganga wafawidhi nendeni mkawasimamie vizuri watoa huduma mwakumbushe wajibu wao kwa kweli hatutawafumbia macho, tunapozungumzia ubora wa huduma ni pamoja na maadili, lugha nzuri na uwajibikaji, "alisema.

Dk. Dugange alisema Ofisi ya TAMISEMI na Rais Samia Suluhu Hassan hawafurahishwi na malalamiko ya wananchi na kuwataka waganga wafawidhi kuhakikisha hayo katika vituo vyao.

"Kuna malalamiko mengine ya kiufundi tunayafahamu, lakini yale ya uzembe hatuvumilia tunajua mkikaa kwenye nafasi zetu tutaondoa au kupunguza malalamiko," alisema.

Naibu Katibu Mkuu kutoka Wizara ya Afya, Dk. Grace Magembe, alisema watumishi wa afya wakitekeleza majukumu yao kikamilifu watakuwa chachu ya kupambana na vifo vya mama na mtoto.

Mwenyekiti wa waganga wafawidhi wa vituo vya afya ngazi ya msingi, Dk.Florence Hilari, aliahidi watatekeleza maagizo ya kutoa huduma bora kwa wananchi.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akizungumza na viongozi wanawake wa Mkoa wa Geita, walipotembelea bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mkalama kutumia bil. 29.9/-

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama mkoani Singida limeridhia Shilingi bilioni 29.966 kutumika kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, mishahara ya wafanyakazi na matumizi mengine kwa mwaka huu wa fedha wa 2024/ 2025.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Asia Messos, akiwasilisha bajeti hiyo jana kwenye kikao cha madiwani hao, alisema maeneo yaliyopewa kipaumbele ni kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kutoka Shilingi bilioni 1.739 ya mwaka uliopita wa 2023/2024 hadi kufikia Shilingi bilioni 2.430 kwa 2024/2025.

Alisema kiwango hicho ambacho ni ongezeko la Shilingi milioni 691.388 sawa na asilimia 39.7.

Alisema katika bajeti hiyo, Shilingi bilioni 3.576 zitatumika kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alivitaja vipaumbele katika bajeti hiyo kuwa ni kukamilisha miradi inayoendelea kutekelezwa ili iweze kutoa huduma kabla ya kuanza mipya na ulipaji malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa umma.

Alivitaja vipaumbele vingine kuwa ni kutenga bajeti kwa ajili ya kutoa elimu ya uhamasishaji kwa wakulima, wafugaji na wavuvi kushiriki katika ujenzi wa miundombinu hiyo na stahiki za watumishi ambazo ni mishahara, malimbikizo na uhamisho.

Alisema katika bajeti iliyopita ya 2023/2024 kipindi cha Julai hadi Desemba mafanikio yaliyopatikana ni kutekelezwa miradi yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.198 katika sekta ya elimu, kusajili shule mpya za sekondari na kuajiri watumishi wapya 56.

Alisema vilevile kuthibitisha kazini watumishi 44, kuwapandisha vyeo wapya 103 na kuwaendeleza kimasomo 27.

Mkurugenzi huyo, aliwaomba madiwani wasaidie katika usimamizi wa miradi inayoendelea kutekelezwa katika maeneo yao ili iwe tija kwa wananchi.

"Ni ngumu kwa mhandisi kufika kila eneo kwa sababu hivi sasa tuna miradi kila kata na kila kijiji, hivyo madiwani wakitusaidia katika usimamizi itaweza kukamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma kwa wananchi," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, James Mkwega akifunga kikao hicho aliwaomba madiwani kusaidia kutoa ushirikiano wa ukusanyaji wa mapato badala ya kuwaachia watendaji.

Mkwega aliwataka watendaji kupeleka maandiko ya bajeti katika miradi mingi bila kuona aibu kwa ajili ya kupitiwa na kupitishwa kwa ajili ya utekelezaji.

Baada ya bajeti hiyo kuwasilishwa, madiwani walipongeza watendaji wakiongozwa mkurugenzi wa hiyo kwa jinsi wanavyosimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika wilaya hiyo.





# Wajawazito wawekwa kizuizini kwa kushindwa kulipia upasuaji

**Na Elizabeth John,**
MAKETE

WAJAWAZITO wa vijiji vitano vya Kata ya Mfumbi wataondokana na kero ya kuwekwa kizuizini hospitalini kwa kushindwa kulipa gharama za kujifungua watoto kwa upasuaji baada ya Serikali kuanza kuwajengea kituo cha afya kwenye maeneo yao.

Wakinamama hao walisema kitendo cha Serikali kusogeza huduma hiyo pia kutaondoa kero ya kusafiri umbali wa zaidi ya kilomita15 hadi 20 kufuata matibabu kwanye hospitali ya Ilembule, maeneo ya Chimbala na Mbarali Mkoa wa Mbeya.

Mmoja wa wakinamam hao, Hawa Kada, alisema walikuwa wakijifungua mbali na kwa gharama kubwa.

"Hali ambayo ilikuwa ikipelekea wazazi baada ya kujifungua kushindwa kutoa malipo kukaa ndani ya hospitali mpaka watakapotoa malipo, walikuwa wameweka utaratibu wa kibanda chao walikuwa wanaita msonge kama mahabusu ndogo hakuna kutoka kurudi nyumbani hadi utakapolipa hela," alisema Kada.

Halima Sadick, alisema walikuwa wanateseka kufuata huduma ya kujifungua umbali mrefu kutokana na maeneo yao kukosa kituo cha afya.

"Ukifika huko gharama ni kubwa, ukifanyiwa upasuaji inafika hadi shilingi 300,000, ukiwa masikini unafungiwa sero," alisema

Mkurungezi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Makufwe, alisema Serikali imeanza ujenzi wa majengo mawili ya kituo cha afya cha Mfumbi, likiwemo la wagonjwa wa nje yenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni 100.

"Lengo likiwa ni kumaliza adha hiyo ya muda mrefu na huduma za afya ni huduma za msingi kwa wananchi wetu tunahitaji kuboresha ili waweze kushiriki kwenye shughuli za maendeleo," alisema Makufwe.

Baada ya kukagua mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda akiwa na kamati ya ulinzi na usalama alimuagiza mkurugenzi wa halmashauri hiyo kuhakikisha kituo hicho kinaanza kazi mwezi ujao na kupeleka vifaa na wauguzi.



Ofisa Elimu wa Shule za Sekondari wa Manispaa ya Ubungo, Voster Mgina, akifafanua jambo wakati wa ufunguzi wa warsha ya siku mbili kwa Waratibu wa Elimu wa Kata na walimu kutoka shule saba za Dar es Salaam yaliyoandaliwa na Shirika la READ Tanzania juzi, kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa namna bora ya kusimamia maktaba, uhamasishaji wa wanafunzi kutumia maktaba ili kuongeza maarifa na uwezo kitaaluma pia kubadilishana uzoefu na mbinu za kutatua changamoto za uratibu wa maktaba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakiwa kuacha ulevi Kwaresma

**Na Mwandishi Wetu,**
NJOMBE

WAUMINI wa Kanisa Katoliki Jimbo la Njombe mkoani hapa wametakiwa kuachana na ulevi katika kipindi cha mfungo wa Kwaresma.

Wito huo ulitolewa na Askofu Jimbo hilo, Eusebius Kyando wakati wa ibada ya jumatano ya majivu iliyofanyika Kanisa la Mtakatifu Joseph.

Askofu Kyando, alisema waumini wanapaswa kuonyesha utofauti wa kipindi hicho na cha kawaida.

"Itashangaza kumkuta mkristu mkatoliki katika kipindi hiki cha Kwaresma amekunywa pombe anashindwa hata kujua nyumbani kwake ni wapi, tunategemea tutakuwa watu wa kiasi ili kweli kipindi hiki kiwe na matunda ya kufaa kwa ajili ya wokovu wetu," alisema Kyando.

Alisema Kwaresma ni kipindi cha mazoezi ya kiroho na kutenda mema.

"Tujitahidi wala tusionyeshe kwa waziwazi, kupiga propaganda bali tufanye kwa nia kwamba tunaona sura ya Mwenyezi Mungu kwa wale wanaohitaji sura ya Yesu, wale wenye shida tuko tayari kuwasaidia," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka akizungumza katika ibada hiyo, alisema kuwa kwa tathimini ya utafiti wa serikali kupitia taasisi ya Takwimu NBS iliwasilisha taarifa mwaka jana Novemba mkoa huo unaongoza kwa watoto kuwa na udumavu.

"Kinamama 100 wajawazito wakienda hospitali wastani wa 30 wana upungufu wa damu, watoto wa Njombe wana utapiamlo na ukondefu katikati ya neema yote ambayo Mungu ametupatia, " alisema Mtaka.

Mtaka, alisema katika majuma sita ya Kwaresma, jamii kupitia jumuiya zao wanapaswa kukumbushana juu ya malezi ya watoto na kuachana na ulevi.

"WAWATA (Umoja wa Wanawake wa Katoliki Tanzania) waweze kutusaidia huko chini hali mbaya sana wakinamama wa Njombe wanakunywa pombe na wanawanywesha watoto ni utafiti kwa hiyo mama hapati muda wa kuandaa chakula, wa kunyonyesha na mtoto hapati muda wa kula kwa sababu mzazi anaamini akimpatia pombe hatapiga kelele wala kumsumbua," alisema Mtaka.

Baadhi ya waumini wa kanisa hilo, w alisema mfungo huo wa Kwaresma ni muhimu kwa sababu ni nafasi ya kutubu dhambi na kusamehewa.

"Ni siku nzuri kwa sababu ni siku ya kukombolewa sisi Wakristo na kubwa tunalokwenda kulifanya ni kujitenga na dhambi ambayo inatufanya tusiwe wafuasi kwa sababu Yesu Kristo mwenyewe alifunga siku 40, " alisema Isack Mlelwa.

Alisema waumini wanapaswa kufuata nyayo za Yesu Kristo kwa kufunga na kufuata yale yote yanayoelekezwa na viongozi wa dini.

## Wanakijiji Njombe wateka maji Mbeya

**Na Mwandishi Wetu,**
WANGING'OMBE

WAKAZI wa Kijiji cha Lyamluki Kata ya Kijombe wilayani hapa Mkoa wa Njombe wameiomba Serikali kuwapatia maji safi na salama na kuondokana na kero kwenda kuteka maji Bonde la Mto Ruaha lililopo Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wakazi hao, walisema wanakabiliwa na changamoto ya maji huku wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kata Kijombe wakilazimika kucha masomo kwenda kutafuta maji kwenye bonde hilo lililopo umbali wa kilomita tisa.

Riziki Homange, alisema kutokana na kutumia muda mwingi kufuata maji, wanawake wengi wanashindwa kuwaandalia chakula watoto wao kwa wakati na kusababisha kuibuka migogoro ya ndoa kutokana na kuchelewa kurudi nyumbani.

"Hususani Kata ya Kijombe pale sekondari watoto wanaenda na dumu na kindoo kwenda kuchota bondeni wapate kuoga na kufulia nguo," alisema Homange.

Rahabu Mlawa alisema: "Maji kwa mwezi tunaweza kupata maji mara moja au mara mbili, tunaiomba Serikali itusaidie," alisema.

Damson Sikumbili, alisema mabomba yapo lakini maji hakuna hawajui tatizo liko wapi.

"Humo humo wanakunywa na ng'ombe sisi tunachota, watu wanaingia wanaoga kwa kweli kiusalama hali ni ngumu, inafika mahali tunanunua dumu la maji hadi Shilingi 700," alisema Sikumbili.

Diwani wa Kijombe, Seylvester Kigola alithibitisha kuwepo kwa changamoto ya maji katika kata yake na kuahidi kuwa Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha huduma hizo zinapatikana.

Kigola, alisema tatizo hilo litakuwa historia baada ya mradi wa maji wa Igando hadi Kijombe kuanza kutekelezwa.

"Mradi wa Mbukwa wakati unaingia uliingia na idadi ndogo ya watumiaji sasa idadi iliyopo wilayani Wanging'ombe ni kubwa kwa hiyo utashangaa ndani ya wiki moja maji yanatoka mara moja kwa mwezi yanaweza kutoka mara mbili wananchi wanahaki ya kualalamika," alisema Kigola.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Wanging'ombe, Mhandisi Jushi Hamis, alisema wanachimba kisima katika Kijiji cha Iyadebwe na kutekeleza mradi wa Igando hadi Kijombe ili kukabiliana na uhaba wa maji.

"Vijiji viwili kwa maana ya Malangali na Hanjawanu mradi upo karibia asilimia 90 kukamilika, tunachokamilisha ni eneo la Hanjawanu kuna eneo dogo tunamalizia na mabomba tayari tumeshatandika," alisema Hamis.

Alisema serikali imetafuta mkandarasi wa kutekeleza mradi wa maji katika vijiji vitano vya Igando, Kijombe, Iyai, Mayale na Lyadebwe utakaogharimu zaidi ya Shilingi bilioni 10.





## Kilio wakulima wa mwani kukosa soko chamfikia waziri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Shaabani Ali Othman, ameingilia kati kilio cha wananchi wa Kijiji cha Bweleo kuhusu zao la mwani kukosa soko kwa muda mrefu, kunakosababishwa na kampuni inayonunua zao hilo kuacha kununua.

Hatua hiyo imekuja baada wananchi wa kijiji hicho kutoa malalamiko yao juu ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali ikiwemo kukosa soko la zao hilo.

Wananchi waliwataka watendaji kukaa na wanunuzi wa mwani kujua sababu ya kutoendelea na ununuzi wa zao hilo, ili kumaliza kilio cha wananchi cha kukosa soko.

Asha Shaaban Salum ni miongoni mwa wananchi wa kijiji hicho cha Bweleo kilichopo Wilaya ya Magharib 'B' Unguja aliiomba serikali kuwapatia soko la kuuzia mwani, ili waondokane na tatizo la ukosefu wa soko la uhakika la kuuza bidhaa hiyo.

Wakizungumza na watendaji wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi waliofika kijiji hapo jana kusikiliza kero za wananchi alisema wamekosa soko kwa muda mrefu na kushindwa kujua sehemu sahihi ya kuuza bidhaa ya mwani.

Alisema kukosa eneo sahihi la kuuzia bidhaa ni kuendelea kukosa huduma na familia zao kutokana na kushindwa kupata mahitaji.

Mkulima mwingine wa mwani, Wanu Saleh, alisema licha ya kuendelea na kulima mwani, lakini hawana soko la uhakika la kuuza na kusababisha mwani kubakia majumbani mwao.

Alisema tatizo la kukosa soko la kuuzia mwani limesababisha wakulima kutokuwa na imani ya kuendelea na kilimo hicho.

Hivyo wakulima hao waliitaka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kufuatilia tatizo lililojitokeza kwa muwekezaji ambaye alijitokeza kununua mwani na kusitisha zoezi hilo na pia kuwapatia soko lingine ili wauze bidhaa hiyo.

Mkulima Safia Hashim Makame, aliiomba Wizara kuwapatia maeneo ya ujenzi wa mabwawa ya kufugia majongoo bahari ili kupata mavuno.

Waziri Shaabani akitoa majibu ya malalamiko hayo aliishauri kamati ya Kijiji cha Bweleo kwa kushirikiana na watendaji wa Bweleo kutafuta eneo la kuanikia mwani ili kuondosha tatizo la wakulima la kuanika mwani kando ya barabara.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema tenda ya kununua mwani, ilichukuliwa na kampuni ya ZASCO, endapo imesitisha wizara itawafuatilia watendaji wa kampuni hiyo.

# Spika amwapisha aliyeteuliwa na Dk. Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid amemwapisha, Sharif Ali Sharif kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi baada ya kumteua hivi karibuni.

Kabla ya uteuzi huo, Sharif alikuwa ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), alikula kiapo hicho jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Katika kikao hicho Spika Zuberi pia alitoa taarifa kuhusu miswada ya sheria iliyopitishwa katika Mkutano wa 13 wa Baraza hilo na kuwa sheria kamili, baada ya kusainiwa na Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi.


"Katika mkutano huo, baraza lilipitisha miswada sita ya sheria ambayo ni Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya kuanzisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Namba. 11 ya 2003 na Kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Umma na kuweka mambo mengine yanayohusiana na hayo" alisema.

Alisema pia Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Namba. 9 ya 2017 na kutunga Sheria ya Mahakama za Kadhi na kuweka mambo mengine yanayohusiana na hayo na Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Utoaji Leseni, kudhibiti na kusimamia biashara ya huduma ndogo za fedha kwa ajili ya kudumisha utulivu, usalama na ubora wa huduma ndogo fedha na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Aidha alisema mswada mwingine uliosainiwa na kuwa sheria kamili ni Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Namba. 14 ya Mwaka 2018 na kutunga Sheria ya Uwekezaji Zanzibar na kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo.

Pia alisema Mswada wa Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar na kuweka mambo mengine yanayohusiana na hayo na Mswada wa Sheria ya kuanzisha Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar kwa ajili ya ununuzi, utengenezaji, uhifadhi na usambazaji wa dawa na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Spika Zuberi alisema: "Kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 92(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020; naomba kutoa taarifa kwamba miswada hiyo niliyoitaja, sasa imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi".



Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Maulid (kulia), akimwapisha Sharif Ali Sharif kuwa Mjumbe wa baraza hilo, Chukwani jana, baada ya kuteuliwa hivi karibuni na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuwa mjumbe wa baraza hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri: Utawala bora Zanzibar umeimarika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman amesema dhana ya utawala bora imeimarika visiwani Zanzibar.

Amesema maeneo mengi ya kiuendeshaji kama vile ya kiutawala, masuala ya haki za binaadamu pamoja na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Ameir Abd Ameir aliyetaka kujua kwa kiasi gani dhana ya utawala bora imezidi kuimarika katika Serikali ya sasa.

Waziri Haroun alisema serikali inaendelea kuimarisha taasisi mbalimbali zikiwemo, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA) kwa kuwapatia jengo na vifaa vya kisasa jambo ambalo limepelekea kuimarika kwa udhibiti na uzuiaji wa vitendo vya rushwa nchini.

Alisema pia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nayo pia imeimarisha dhana ya utawala bora kupitia mifumo ya utoaji wa ripoti zake.

"Hivi sasa ripoti za CAG zinawasilishwa hadharani mbele ya viongozi na wananchi na zinarushwa mubashara kupitia vyombo vya habari kwa lengo la kuwawezesha wananchi kufahamu matumizi halisi ya fedha zao" alisema.

Alisema Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma pia inaendelea kuimarisha fomu ya tamko la mali na madeni ya viongozi wa umma ili kuhakikisha maadili katika utumishi wa umma yanaimarika kwa kila hatua.


Aidha alisema Wakala wa Serikali Mtandao nayo imeanzisha mifumo mbalimbali ya kielektroniki ikiwemo ofisi mtandao, mfumo wa manunuzi, mfumo wa ZANMALIPO na mfumo wa kutolea risiti za kielektroniki (VFMS) na kuwepo kwa mifumo hiyo kumesababisha kupungua kwa urasimu wa upatikanaji wa huduma za Serikali, kudhibiti mapato na kuwepo kwa utaratibu wa kupata taarifa kwa wataka huduma.

Hata hivyo alisema katika kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma, Serikali imeanzisha Mfumo wa Kielektoniki wa Sema na Rais (SNR) ambao unawawezesha wananchi kutoa malalamiko yao na kufanyiwa kazi kwa umakini na uharaka.

Alisema pia uanzishwaji wa utaratibu wa Rais kuzungumza na waandishi wa habari kila mwisho wa mwezi ili kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi za shughuli za maendeleo na mambo mengine yaliyotekelezwa na Serikali kumesaidia kuimarisha uwazi na uwajibikaji nchini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ABBY ALLY JUMA** anatangaza kupotelewa kwa hati ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE256878 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 15/12/2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/21170/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI TREKTA

**MOHAMEDI KAAYU PARSEKO,**

Anatangaza kupotea kwa kadi ya Trekta aina ya SWARAJ 744EA Yenye no za usajili T353CRB, CHASIS NO WRCL45605181592, ENGINE NO 431025SSK13901.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

**TAARIFA YA POLISI: PHQ/MAN/KIT/857/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

**ANGETILE MWANTEMBE MWAKAJUMBA** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 948 CLZ** aina ya Idapa **JOB 5DGBO5365.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ MBE/RUN/8424/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 25/2024**
**Jina la Mdai: DIAMOND TRUST BANK**
**Jina la Mdaiwa: PETER NKENZIE**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)

Kwa: **PETER NKENZIE**

Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba **FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe **19/02/2024 saa 5:30** asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama itaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe ......Mwezi....Mwaka .....

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 30/2024**
**Jina la Mdai: DIAMOND TRUST BANK**
**Jina la Mdaiwa: CONSTANCIA MANACE SHIRIMA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)

Kwa: **CONSTANCIA MANACE SHIRIMA - 0766507413**

Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba

**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe **06/02/2024 saa 3** asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama itaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **8 Mwezi 2 Mwaka 2024**

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 27/2024**
**Jina la Mdai: DIAMOND TRUST BANK**
**Jina la Mdaiwa: NASHONI ELIAS NDITUYE**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)

Kwa: **NASHONI ELIAS NDITUYE - 0756167748**

Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba **FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe **26/02/2024 saa 3 asubuhi** kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama itaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **8 Mwezi 2 Mwaka 2024**

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 29/2024**
**Jina la Mdai: DIAMOND TRUST BANK**
**Jina la Mdaiwa: NICHOLAUS ANANIA HAULE**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)

**Kwa: NICHOLAUS ANANIA HAULE - 0758857578**

Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba **FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe **26/02/2024 saa 3 asubuhi** kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama itaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **8 Mwezi 2 Mwaka 2024**

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 23/2024**
**Jina la Mdai: DIAMOND TRUST BANK**
**Jina la Mdaiwa: STELLAH MAGOGO**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)

Kwa: **STELLAH MAGOGO**

Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba **FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe **19/02/2024 saa 11:00 asubuhi/Mchana** kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama itaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe ...... Mwezi .... Mwaka .....

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 22/2024**
**Jina la Mdai: DIAMOND TRUST BANK**
**Jina la Mdaiwa: AWADH FAKI MJAKA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)

Kwa: **AWADHI FAKI MJAKA**

Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba **FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe **20/02/2024 saa 11 asubuhi/Mchana** kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama itaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe .....Mwezi .... Mwaka ........

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 2712 / 2023**
**In the matter of the Estate of the late VAILETI DAVID SONYO of Miyuji Ward within City Council of Dodoma**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY BARAKA ALEX MJANJA**

### GENERAL CITATION

**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 15 Day of March, 2024

**Dated at Dodoma this 14 Day of 02, 2024**

RESIDENT MAGISTRATE

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

### Blinken ataka uchaguzi Senegal ufanyike haraka

**WASHINGTON,** MAREKANI

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, amehimiza kuendelea na mchakato wa kufanyika kwa uchaguzi mkuu nchini Senegal kama ulivyopangwa.

Blinken alizungumza na Rais wa nchi hiyo, Macky Sall kuwa uchaguzi huo ufanyike haraka iwezekanavyo na kuonyesha wasiwasi wake kuhusu hatua ya kuahirishwa.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje, Matthew Miller, alisema katika mazungumzo hayo kwa njia ya simu aliweka wazi kuwa wangependa kuona uchaguzi unafanyika kama ulivyopangwa.

Miller alisema Marekani ina wasiwasi kuhusu hali katika taifa hilo la Afrika Magharibi baada ya serikali kuzuia mitandao ya simu na kupiga marufuku maandamano.

Aliongeza kuwa Blinken alihimiza uchaguzi ufanyike kwa wakati na ikiwa hautafanyika Februari 25, ungepaswa kupangwa tarehe za karibuni.

Rais Sall alisogeza mbele uchaguzi wa Februari 25, na kusababisha mzozo wa kisiasa nchini humo, ambako awali ilisifika kuwa na demokrasia bora barani kwa Afrika.

Katika hatua inayofanana na hiyo, Msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, alisema lazima iheshimiwe haki ya kuandamana kwa raia wa Senegal.

Kauli hiyo imetolewa baada ya serikali kupiga marufuku maandamano kutokana na kuahirishwa kwa uchaguzi wa rais.

Msemaji wa Guterres, Stephane Dujarric alisema wana wasiwasi kuhusu hali ya amani nchini Senegal.

Aidha alisema ni muhimu kwa Wasenegal wote wawe na haki yao ya kuandamana, kuheshimiwa na kataka hali kutoelewana kati ya serikali na upinanzani isuluhishwe kupitia njia zilizowekwa za kikatiba. **DW**



# Hofu yazidi kutanda kuvamiwa Rafah, Afrika Kusini yakimbilia mahakamani

**GAZA,** PALESTINA

WAKATI nchi ya Afrika Kusini imewasilisha ombi la dharura katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki ikitaka kuzuia shambulizi lolote kutoka kwa Israel, Umoja wa Mataifa umeonya hatua yoyote ya kuipiga Rafar itakua mauaji ya alaiki.

Katika taarifa iliyotolewa na serikali ilieleza mashambulizi ya Israel dhidi ya Rafah yanaweza kusababisha ukiukwaji zaidi wa haki za Wapalestina, Gaza.

Serikali ya Afrika Kusini ilisema katika ombi lake hilo kuwa ina wasiwasi kuhusu uwezekano wa mauaji makubwa zaidi.

Mwezi uliopita, Mahakama ya Kimataifa ya Haki iliiamuru Israel kuchukua hatua zote zinazowezekana kuzuia vitendo vitakavyoleta mauaji ya kimbari dhidi ya raia wa Kipalestina.

Aidha, nchi hiyo ilisisitiza kwamba kuanzisha kwa mashambulizi makubwa katika eneo la Rafah itakuwa ni ukiukaji wa Mkataba wa Mauaji ya Kimbari.'

Wakati huo huo, ofisa wa ngazi ya juu wa Umoja wa Mataifa ameonya shambulio lolote la Israel dhidi mji huo ulioko kusini mwa Gaza, huenda likasababisha mauaji yasiyoelezeka.

Mkuu wa masuala ya kibinadamu Martin Griffiths, alisema kwamba Wapalestina wanaoishi katika mji wa Gaza tayari wanateseka kutokana na mashambulizi yasiyo na mfano, na ukatili mbaya zaidi.

"Matokeo ya uvamizi wa Rafah yatakuwa janga", alisema.

Hata hivyo, Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, ameapa kuwashinda wapiganaji wa Hamas ambao alisema wamejificha katika mji huo.

Katika taarifa yake yenye maneno makali , Griffiths alisema zaidi ya watu milioni moja wamejazana katika mji wa Rafah, wakitazama kifo kikiiwajia usoni.

Alisema raia katika jiji hilo wamebakiwa na chakula kidogo na upatikanaji huduma za matibabu wa kiwango cha chini na hakuna mahali salama pa kwenda.

Aliongeza kuwa uvamizi wa Israeli katika mji huo, utaacha watu wengi wakiwa karibu na kifo kutokana na operesheni ya kibinadamu kudhoofika.

Msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, alikiambia kipindi cha BBC cha Newshour kuwa chombo hicho hakitapokea mpango wowote wa kuwahamisha watu kutoka Rafah unafanyiwa kazi na Israel, na kusisitiza hautashiriki katika uhamishaji wowote wa lazima.

**BBC**




Wananchi wakihama maeneo yao kwenda sehemu salama baada ya mapambano makali kushuhudiwa katika mji wa Sake. **PICHA: AFP**

# Waasi M23 wanakaribia kuuteka mji wa Sake

**GOMA,** DRC

MAPIGANO makali yanaendelea kwenye vilima vinavyoelekea eneo la Sake na kusababisha taharuki kwa wananchi wanaoishi katika mji wa Goma, mkoa wa Kivu Kaskazini mashariki mwa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Hata hivyo jeshi la serikali lilisema licha ya mapigano hayo, wanaendelea kuidhibiti mji wa Sake.

"Watu wamekimbia eneo hilo, mji ulikuwa na idadi kubwa ya watu hapo awali " alisema Meya wa mji huo Maombi Mubiri.

"Kwa sasa, waasi wanakalia sehemu ya kusini ya jiji, wakati wazalendo (wanamgambo wanasaidia jeshi la DRC) wako katika sehemu ya kaskazini," aliongeza.

Kulingana na chanzo kutoka hospitali ya mji huo, milio ya risasi ya hapa na pale ilisikika katika mji huo na hospitali imepokea watu watatu waliojeruhiwa kwa risasi.

Tangu mwisho wa mwaka 2021, mkoa wa Kivu Kaskazini umekumbwa na mzozo kati ya M23, inayoungwa mkono na Rwanda, na jeshi la serikali ya DRC ikishirikiana na vikundi vyenye silaha na kampuni mbili za kijeshi kutoka nje.

Waasi wa M23 wanatuhumiwa kutumia silaha za kisasa kama vile makombora ya Sol-air, kulingana na waraka wa Umoja wa Mataifa na shirika la habari AFP ilipata nakala yake.

Akiwasili mjini Goma juzi katika ziara yake ya pili Waziri wa Ulinzi, Jean-Pierre Bemba, alihakikisha kwamba kila kitu kinafanyika ili kulinda wakazi wa Sake, Goma na maeneo yote jirani.

Juhudi mbalimbali za kidiplomasia zilizoanzishwa kujaribu kutatua mgogoro huu hazijafanikiwa hadi sasa. Juzi rais wa Burundi alitangaza katika vyombo vya habari kwamba Rais Évariste Ndayishimiye anasafiri kwenda DRC kama utekelezwaji wa makubaliano kuhusu kushauriana suala la amani katika eneo hilo.

# TWIGA STARS MATUMAINI 'KIBAO' IKIWAALIKA SAUZI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Bakari Shime, amesema kikosi chake kinaendelea vizuri na maandalizi na anaimani watapata matokeo mazuri katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki, imeelezwa.

Twiga Stars itaikaribisha Afrika Kusini katika mchezo wa kwanza utakaochezwa Februari 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na marudiano yakitarajiwa kufanyika baada ya wiki moja.

Tayari Twiga Stars imeshaingia kambini kujiandaa na mechi hizo mbili zilizoko mbele yao.

Akizungumza na Nipashe jana, Shime, alisema wachezaji wote wamefika kambini na wanaendelea na programu ya mazoezi aliyoiandaa na anafurahi kuona viwango vya nyota wake vinaimarika.

Shime alisema ushindani ulioko katika ligi mbalimbali wanazocheza wachezaji wake umesaidia kuimarisha viwango vyao na hii inasaidia kuwapa matokeo chanya.

„Mipango yetu sasa ni kujiandaa vizuri kwa ajili ya kusaka ushindi mbele ya wapinzani (Afrika Kusini), tutakaokutana nao, tunatambua hakuna mechi rahisi hasa katika hatua hii, tunahitaji kufanya vizuri, tunahitaji matokeo mazuri na kufikia lengo, ni lazima tufanye maandalizi mazuri pia," alisema Shime.

Aliwataja wachezaji wanaojiandaa na mechi hiyo ni pamoja na Najiat Abbasi (JKT Queens ), Asha Mrisho (Amani Queens), Husna Mtunda (Yanga Princess), Julietha Singano (Juarez, Mexico), Anastazia Katunzi, Christer Bahera, Happy Hezron (JKT Queens), Fatuma Issa ,Fetty Densa' na Violeth Nicholaus wote kutoka Simba Queens.

Wengine ni pamoja na Ester Mabanza, Stumai Abdallah, Joyce Lema, Janet Christopher, Amina Bilali (JKT Queens), Aquila Gaspar (Fountain Gate Princess) Hasnat Ubamba, Irene Kisisa (Yanga Princess), Enekia Kasonga (Eastern Flames- Saudia Arabia) na Diana Lucas anayekipiga katika klabu ya Ame S.F.K ya Uturuki.

Washambuliaji walioko katika kikosi hicho ni Opa Clement anayecheza Besiktas iliyoko Uturuki , Aisha Juma (Simba Queens), Donisia Minja, Winifrida Gerald na Jamila Rajabu wa JKT Queens.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Dar es Salaam wakicheza mpira wa kikapu kwenye viwanja vya JMK Park jijini, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mashujaa yaionya Kagera Sugar

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Mashujaa FC, Mohamed Abdallah ,Bares' amesema Kagera Sugar itakuwa katika wakati ,mgumu' tofauti na mechi mbili zilizopita walipocheza dhidi ya Yanga na Singida United katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kagera Sugar itawaalika Mashujaa kesho kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba mkoani, Kagera.

Bares ameikumbusha Kagera Sugar wao ni timu tofauti na wamejipanga kushuka dimbani wakiwa na mbinu mbadala.

Kocha huyo alisema amewataka wachezaji wake kuongeza utulivu katika mechi hiyo ya kwanza ya mzunguko wa pili ili kuvuna pointi tatu muhimu.

„Kagera Sugar imekuwa na matokeo mazuri siku za hivi karibuni na watataka kuendeleza, na sisi tumetoka kwenye matokeo ambayo si mabaya sana, tutakachohakikisha ni kucheza kwa nidhamu, wachezaji wetu kujituma kuhakikisha tunaondoka na ushindi ili hata kama hatatutoa sana chini ya msimamo lakini kutakuwa na mwelekeo mzuri wa kwenda juu," alitamba Bares.

Kocha huyo alikiri timu yake iko katika nafasi mbaya kwenye msimamo hivyo anataka kuona wanajiondoa katika nafasi hiyo kwa kupata ushindi au kugawana pointi.

Ligi Kuu Bara inatarajia kuendelea tena leo kwa JKT Tanzania kuwakaribisha Simba kwenye Uwanja wa Isamhuyo ulioko Mbweni, Dar es Salaam.

# Zimamoto, Hard Rock majaribuni

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

ZIMAMOTO SC inatarajia kukutana na Wanajeshi wa Hard Rock kutoka Pemba katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mau A.

Kocha Mkuu wa Zimamoto, Ali Mohamed ,Tedy', aliliambia gazeti hili licha ya kupoteza mechi mbili zilizopita, anatarajia timu yake itafanya vyema katika mchezo wa leo na kujiimarisha katika ligi hiyo.

Tedy alisema ingawa anaamini mechi hiyo itakuwa ngumu, kwa upande wake amejipanga kuhakikisha anapata alama tatu muhimu na kuendelea na mikakati ya kuwania ubingwa.

Kocha huyo alisema kupoteza michezo iliyopita ya mzunguko wa kwanza hakujawaondoa katika ndoto zao za kutwaa ubingwa na bado anamatumaini ya kuvuna pointi kwenye michezo 13 iliyobakia.

Alisema changamoto kubwa iliyopo katika timu yake hivi ni safu ya ulinzi na kukosa utulivu kwa washambuliaji wale, hivyo anaendelea kufanyia kazi ili kumaliza changamoto hiyo.

„Tunawajenga na kuwapa mbinu mpya washambuliaji wetu, tunataka kuona wanafanya maamuzi ya haraka hasa pale wanapopata nafasi ya kushambulia lango la wapinzani wetu.

Bado tatizo la umakini na maamuzi ya haraka ni changamoto kubwa katika michezo hii miwili iliyopita, tunashindwa kuzitumia nafasi tunazopata lakini pia walinzi nao kuna muda wanazidiwa ujanja, tumeendelea kujinoa ili kumaliza changamoto hizi," alisema Tedy.

Aliongeza wanawaheshimu wapinzani wao ambao pia anaamini watashuka dimbani wakiwa na malengo ya kupata alama tatu wakiwa ugenini hivyo wachezaji wake wanatakiwa kuwasoma na kujiandaa kukabiliana na ugumu huo.

"Lazima tuingie uwanjani na mbinu ambayo itakayotupa sisi ushindi katika mchezo huu kwa sababu tunajua mechi haitakuwa rahisi kwa kila upande," Tedy aliongeza.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Zimamoto iko katika nafasi ya nne ikiwa na pointi 30 wakati vinara ni JKU yenye pointi 39 wakifuatiwa na KMKM yenye pointi 35 na KVZ waliojikusanyia pointi 33 hadi sasa.

## ZISIKUPITE

### GALLAGHER AWANIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur itamnunua Conor Gallagher wa Chelsea msimu huu wa joto ikiwa kiungo huyo wa England mwenye umri wa miaka 24 hataafikiana na The Blues hao kuhusu kuongeza mkataba wake wa sasa, ambao unamalizika mwishoni mwa msimu ujao. **(Telegraph)**

### TONEY AWINDWA ARSENAL

KLABU ya Arsenal na Newcastle United zipo macho baada ya mazungumzo ya mkataba mpya kati ya Brentford na mshambuliaji wao wa England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27. **(TeamTalk)**

### DAVID MBADALA WA TONEY

KLABU ya Brentford imemtambua mshambuliaji wa Lille na Canada, Jonathan David mwenye umri wa miaka 24, kama mbadala wake iwapo Ivan Toney ataondoka katika klabu hiyo msimu huu wa joto. **(Football Transfers)**

### BRANTHWAITE AWA LULU

MANCHESTER United na Tottenham Hotspur inafanya bidii zaidi kumsajili Jarrad Branthwaite wa Everton, huku klabu za Chelsea, Arsenal na Real Madrid zikimuulizia beki huyo wa England mwenye umri wa miaka 21**. (Mail)**

### SAVIO AKARIBIA MAN CITY

MANCHESTER City imekubali mkataba wa kumnunua winga wa Brazil, Savio mwenye umri wa miaka 19, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu ya Girona ya Hispania. **(Fabrizio Romano)**

### GUDMUNDSSON AWANIWA

NEWCASTLE United wameungana na West Ham katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Genoa raia wa Iceland, Albert Gudmundsson mwenye umri wa miaka 26. **(Gazzetta dello Sport)**

### KAI HAVERTZ KUUZWA

ARSENAL inafikiria kumuuza kiungo wa kati wa Ujerumani, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 24 msimu huu wa joto. **(Fichajes)**

### MUDRYK ALITAKIWA MUNICH

KLABU ya Bayern Munich ilitaka kumsajili Mykhailo Mudryk kwa mkopo Januari, lakini Chelsea hawakuwa na nia ya kumruhusu winga huyo wa Ukraine mwenye umri wa miaka 23 kuondoka. **(Fabrizio Romano)**

### ASHWORTH ALENGWA

MKURUGENZI wa michezo wa Newcastle, Dan Ashworth analengwa na Manchester United kuchukua nafasi ya John Murtough, ambaye anatarajiwa kuacha nafasi yake kama mkurugenzi wa soka mara tu dili la Sir Jim Ratcliffe la kununua asilimia 25 ya hisa za Mashetani wekundu hao litakapokamilika**. (I)**

### TUCHEL ATAJWA BARCA

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel yuko kwenye orodha ya makocha wanaopigiwa upatu na Barcelona kurithi mikoba ya Xavi wakati kiungo huyo wa zamani wa Hispania atakapojiuzulu mwishoni mwa msimu huu. **(Sport)**

### MBAPPE ALITAKIWA LIVERPOOL

WAWAKILISHI wa Kylian Mbappe waliwasiliana na Liverpool kuhusu uhamisho mwaka jana, lakini klabu hiyo haikutaka kuvuruga mkakati wao mzima wa kifedha ili kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 25 wa PSG ya Ufaransa. **(Independent)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BRAHIM DÍAZ: BAO LANGU NI MAALUM KWA BELLINGHAM

Mhispania huyo ameweka wazi kuvutiwa na uwezo wa nyota huyo ambaye kwa sasa yupo nje kwa....

**MADRID, Hispania**

BRAHIM Díaz alimsifu mchezaji mwenzake wa „daraja la kimataifa" Jude Bellingham baada ya kufunga bao katika ushindi wa 1-0 wa Real Madrid katika mchezo wa mkondo wa kwanza wa hatua ya 16 bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya RB Leipzig, Jumanne.

Díaz aliiweka Madrid mbele katika dakika ya 48 kwa bidii ya kipekee, akikimbia kwenye safu ya ulinzi ya Leipzig kabla ya kumpita kipa Péter Gulácsi, na kupelekea Bellingham kuandika „Oh my god Brahim!" kwenye mitandao ya kijamii.

Winga huyo wa Hispania alitoa pongezi kwa Bellingham ambaye anatarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa wiki tatu kutokana na kuteguka kwa kifundo cha mguu katika ushindi wa 4-0 wa Madrid dhidi ya Girona siku ya Jumamosi.

„Nampenda Bellingham," alisema Díaz akiiambia Movistar.

„Tangu dakika ya kwanza tumekuwa tukielewana sana, namsaidia kumfundisha lugha ya Kihispania. Ni mchezaji wa kiwango cha kimataifa, nafurahia kucheza naye. Mbali na haiba aliyonayo, ni mtu mzuri sana.

„Licha ya kukosekana kwa Jude na Antonio Rudiger, na wale wachezaji ambao wako nje ya uwanja kwa muda mrefu, tunaendelea kuonesha kwamba sisi ni timu kubwa, kwamba sisi ni Real Madrid."

Díaz alianza msimu akihangaika kuingia katika timu ya Madrid baada ya kusajiliwa kutoka AC Milan, lakini amezidi kuwa muhimu na sasa amefunga mabao nane katika mashindano yote.

„Nilipata mpira, nikaanza kukimbia na nikaona walikuwa na wasiwasi wa kuruka ndani, walikuwa wakirudi nyuma na nikauweka wavuni," alisema Díaz.

„Baada ya miaka miwili akiwa Milan anaonekana kuwa na nguvu, na tabia ya kujituma zaidi," kocha Carlo Ancelotti alisema, alipoulizwa kuhusu Díaz.

„Alianza msimu bila kucheza sana, lakini anapopata nafasi, huwa anachangia. Leo alifunga bao la kuvutia."

Vinara wa LaLiga Madrid sasa watacheza na Rayo Vallecano, Sevilla na Valencia kwenye ligi kabla ya marudiano dhidi ya Leipzig Uwanja wa Santiago Bernabeu Machi 6.

HABARI MICHEZO

# GUARDIOLA AKUNA KICHWA KWA JACK GREALISH, SILVA

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola ameachwa katika wakati mgumu baada ya Jack Grealish na Bernardo Silva kuchechemea wakati Manchester City wakiibuka na ushindi wa 3-1 katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya FC Copenhagen, Jumanne.

Grealish, aliyeanza mchezo kwa mara ya kwanza ndani ya zaidi ya mwezi mmoja, alibadilishwa baada ya dakika 21 tu kutokana na tatizo la paja huku Silva, aliyeifungia City bao la pili, aliumia kwenye kifundo cha mguu katika kipindi cha pili.


City watamenyana na Chelsea kwenye Uwanja wa Etihad Jumamosi na kukabili mwezi muhimu wa Machi kwa mechi dhidi ya Manchester United, Liverpool, Brighton na Arsenal.

"Sikuzungumza na daktari lakini inaonekana Jack aliumia misuli," alisema Guardiola.

"Siku chache zilizopita hali yake katika mazoezi ilikuwa bora zaidi.

"Alihisi kwenye nyasi na kuanza kulalamika. Wachezaji wanaweza kuhisi mara moja ikiwa ni misuli. Alitaka kuendelea, lakini hatukutaka kufanya hali kuwa mbaya zaidi."

Guardiola amewakaribisha Kevin De Bruyne na Erling Haaland kwenye kikosi chake, lakini kiungo Mateo Kovacic na mlinzi Josko Gvardiol hawakuweza kusafiri kwenda Denmark kwa sababu ya majeraha.



"Josko ana wiki mbili au tatu nje. Wameumia kifundo cha mguu, Kova anaweza kurejea, Kila mchezo na kipindi cha mazoezi tunapoteza wachezaji na hiyo si nzuri."

Majeraha kwa Grealish na Silva yalikuwa pigo kwa Guardiola usiku wakati City ilipopiga hatua kubwa kuelekea robo fainali ya Ligi ya Mabingwa.

De Bruyne alifunga bao la kwanza kabla ya kuwatengenezea mabao Silva na Phil Foden na kuwapa mabingwa hao watetezi faida kubwa kabla ya mechi ya mkondo wa pili jijini Manchester Machi 6.

"Najua jinsi ilivyo ngumu," alisema Guardiola.

"Ni mpinzani mgumu sana. Tumeunda dhana kamili leo. Kazi yangu ni kuwaonya wachezaji kuhusu sifa walizonazo.

"Tulijiendesha kwa tabia, utu na uvumilivu, kila mtu alikuwa katika kiwango cha juu. Sio maamuzi lakini ni matokeo mazuri, tunatumahi tunaweza kutinga robo fainali."

## Xabi Alonso aongoza wanaotakiwa Liverpool

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL wameunda orodha fupi ya makocha saba katika kutafuta mrithi wa Jurgen Klopp, huku jina la bosi wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso likiongoza, kwa mujibu wa 90min.

Klopp alitangaza mwishoni mwa Januari kwamba ataondoka Liverpool msimu huu wa joto, jambo ambalo lilishangaza ulimwengu wa soka.

Liverpool pia wana nafasi ya Mkurugenzi wa michezo na 90min inaelewa kuwa klabu ingependelea kupata mgombea hapa kabla ya kuelekeza uangalifu wao kamili kwa hali ya kocha na mshahara huo kwenye bodi.

Hata hivyo, klabu hiyo imekuwa na miezi miwili ya kufanya uangalizi wake kuhusu mbadala wa Klopp baada ya kuwafahamisha kuhusu uamuzi wake huo kwa faragha Novemba mwaka jana.

Vyanzo vimeithibitishia 90min kwamba Alonso ndiye anayeonekana kuwa kinara kwenye orodha hiyo.

Alonso angependa kurejea Liverpool kama kocha, lakini kwa sasa analenga kujaribu kuwapa Leverkusen taji lao la kwanza kabisa la Bundesliga, kwa sasa wanaongoza msimamo kwa pointi tano zaidi kwenye msimamo baada ya ushindi wao wa mabao 3-0 dhidi ya Bayern Munich Jumamosi.

Liverpool sio klabu pekee ya zamani ya Alonso inayovutiwa na kazi yake, huku Real Madrid wakifahamu Carlo Ancelotti hatakuwepo milele licha ya kusaini mkataba mpya hivi karibuni na mustakabali wa Thomas Tuchel katika klabu ya Bayern ukitiliwa shaka hata kama yuko salama kwa sasa.

Roberto De Zerbi wa Brighton & Hove Albion na kocha wa timu ya taifa ya Ujerumani, Julian Nagelsmann pia wako katika ushindani mkali, kama vile kocha mkuu wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou, ambaye alikuwa shabiki wa Liverpool tangu utotoni.

Ruben Amorim wa Sporting CP pia ametajwa katika orodha hiyo pamoja na Unai Emery wa Aston Villa na Roger Schmidt wa Benfica.




## Mo Salah arejea mazoezini Liverpool

**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah alionekana akiwa amerejea katika mazoezi ya Liverpool siku ya Jumanne huku mshambuliaji huyo wa Misri akikaribia kurejea kutokana na jeraha la misuli ya paja.

Salah alipata jeraha hilo mapema katika Kombe la Mataifa ya Afrika, AFCON, ambapo alikumbwa na utata aliporejea Liverpool kwa matibabu na alilazimika kukataa hadharani madai kwamba alikuwa ameliacha taifa lake.

Mpango ulikuwa Salah kurejea AFCON baadaye katika kinyang'anyiro hicho lakini kuondolewa kwa mshangao kwa Misri kulimaanisha kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 angezingatia tu kurejea katika utimamu kamili.




Akiwa amekosa mechi nne zilizopita za Ligi Kuu ya England, Salah alirejea mazoezini Jumanne ili kujiunga na maandalizi ya safari ya Jumamosi hii kuelekea Brentford.

Pia walionekana wakiwa mazoezini mlinda mlango Alisson na beki Joe Gomez, ambaye alikosa mchezo wa ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Burnley kutokana na ugonjwa, na beki wa kulia Conor Bradley, ambaye alipewa muda kuwa nje ya timu kwa sababu kibinafsi.

Thiago Alcantara amerejea uwanjani kutokana na jeraha jipya la misuli ambalo alilipata dakika ya tano tu katika mchezo waliofungwa mabao 3-1 na Arsenal ikiwa mechi yake ya kwanza tangu Aprili 2023 huku kiungo mwenzake Dominik Szoboszlai akiwa nje.

Liverpool wamekaa kileleni kwenye msimamo wa Ligi Kuu na kama watapata ushindi kwenye mchezo wa Jumamosi utaongeza presha kwa wapinzani wake wa karibu Manchester City na Arsenal kwa ushindi dhidi ya Brentford.

# SIMBA YATAMBA HAIJATOKA KWENYE MBIO ZA UBINGWA

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI leo itashuka dimbani kumana na JKT Tanzania, mabosi na benchi la ufundi la Simba wamesema bado wapo katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara licha ya kuachwa nyuma na watani zao, Yanga kwa pointi saba.

Simba yenye pointi 33, imecheza michezo 14 na katika msimamo iko kwenye nafasi ya pili wakifuatiwa na Azam FC ambao pia wanalingana michezo wakiwa na pointi 32 wakati mabingwa watetezi, Yanga wanaongoza wakiwa na pointi 40.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, alisema licha ya timu yake kuzidiwa na watani zao, bado wapo kwenye mbio za ubingwa na hawana presha yoyote kutokana na nafasi waliyopo.

„Ligi bado ina michezo mingi, huwezi kusema haiwezekani wakati bado kuna mechi za mzunguko wa pili, tutaendelea kupambana katika kila mchezo kuhakikisha tunavuna alama tatu,“ alisema Benchikha.

Kocha huyo alisema mechi ya leo inakwenda kumaliza michezo yao ya mzunguko wa kwanza na wamejipanga kuhakikisha wanapata ushindi utakaoendelea kuwapa morali kufikia malengo.

„Nina imani na wachezaji wangu, wamekuwa wananipa kile ambacho nawaagiza, tunaangalia michezo yetu zaidi, tunataka tushinde kila mchezo,“ Benchikha alisema.

Kauli hizo za Benchikha ziliopewa nguvu uongozi wa timu hiyo kupitia kwa Meneja wa Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, ambaye alisema bado wanaendelea na mapambano ya kusaka ubingwa wa msimu huu.

„Bado hatujatoka kwenye njia za ubingwa na hatuwezi kutoka, tumeanza kuona manufaa ya usajili wetu wa dirisha dogo kwa wachezaji wa nje, wanatupa kile tulichokuwa tunakihitaji kutoka kwao,“ alisema Ahmed.

Alisema kwa wachezaji wao wa ndani waliowasajili hivi karibuni wanaendelea kuwapa muda na wanaamini watasaidia timu hiyo kutokana na uwepo wao.

Aliongeza Simba hawana hofu yoyote kuelekea mechi dhidi ya JKT Tanzania ambayo itachezwa kwenye uwanja wao wa nyumbani wa Meja Isamuhyo.

„Tunakwenda kufuata alama tatu, hatuiogopi JKT hata wakicheza kwao, tunataka kutimiza lengo letu msimu huu,“ alisema Ahmed.

# Tabora Utd yafunguka ilipokwama

**Na Adam Fungamwango**

MABOSI wa Tabora United wamesema timu yao haikufanya vyema katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara kutokana na kukumbwa na ‚upepo mbaya‘ huku wakiweka wazi hawana changamoto ya ukata ndani ya timu hiyo.

Ofisa Habari wa Tabora United, Christina Mwagala, alisema jana kufanya vibaya kwa timu yao hakuhusiani na suala la madai kwa wachezaji, ukata wa kulipa mishahara, badala yake ni bahati mbaya tu, lakini wana imani watafanya vizuri mzunguko wa lala salama.

„Hatuna changamoto yoyote kama wachezaji wanadai, mishahara inachelewa, hapana wachezaji wetu wanalipwa mishahara kwa wakati, wanalipwa tarehe 23, ikichelewa tarehe 25 kwa hiyo matokeo haya hawawezi kuhusishwa na vitu kama hivyo, hayahusiani, ni upepo mbaya tu umetukumba,“ alisema Mwagala.

Aliwataka mashabiki wa soka Tabora kuiunga mkono na kuahidi kuanza kufanya vizuri mechi za mzunguko wa pili.

„Niwasihi sana mashabiki wa klabu ya Tabora United tushikamane, tuwe kitu kimoja, tuwasapoti vijana wetu, naamini mzunguko wa pili tunakwenda kufanya makubwa katika mechi zetu, kuanzia mchezo dhidi ya Azam,“ Mwagala alitamba.

Mara ya mwisho kwa timu hiyo kupata ushindi ilikuwa ni Desemba Mosi, mwaka jana iliposhinda nyumbani, mabao 2-1 dhidi ya Mtibwa Sugar, lakini baada ya hapo imecheza mechi tano mfululizo.

Tabora United iko kambini kujiandaa kuivaa Azam FC, mechi itakayopigwa Jumatatu kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi huku wakiwa na kumbukumbu ya kufungwa mabao 4-0 katika mchezo wao wa kwanza wa msimu huu.




Kiungo wa Azam FC, Yannick Bangala, akifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga yavunja rekodi Ligi Kuu

INATOKA UK. 24

mabao 2-1 dhidi ya Ihefu, Oktoba 4, mwaka jana, ikicheza ugenini kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya, na ilipotoka suluhu dhidi ya Kagera Sugar.

Kamwe amesema kwa sababu Gamondi ameanza kumtumia Aziz Ki kama namba tisa, basi ana uhakika anaweza kutwaa kiatu cha dhahabu msimu huu, huku akitamba kikosi chao kwa sasa kimekamilika baada ya urejeo wa kipa namba moja, Djigui Diarra.

“Tukumbuke Aziz Ki sasa hivi anatumika kama namba tisa katika kikosi cha Miguel Gamondi, kwa hiyo tunatarajia atafanya makubwa sana msimu huu, na niwatoe hofu wanachama na mashabiki wa Yanga kikosi chetu kwa sasa kimekamilika, kambini kuna wachezaji wote, Diarra pia amesharejea.

Sasa tumekamilika, nadhani baada ya kufanya vizuri katika mzunguko wa kwanza, sasa tunataka kufanya vyema zaidi mzunguko wa pili kwa ajili ya kuupata ubingwa,“ aliongeza ofisa huyo.

Alisema pia ligi msimu huu imekuwa ngumu, lakini akiihofia zaidi Azam FC ambayo inaonekana imeongeza zaidi ushindani, hivyo kuwataka wanachama na mashabiki kuungana.

„Tunatakiwa kuimarika zaidi, tunatakiwa kuungana kuwa kitu kimoja,“ Kamwe alisema.

Diarra ndiye mchezaji wa mwisho wa timu hiyo kurejea, akiwa ametoka katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) yaliyofanyika Ivory Coast, akiiwakilisha nchi yake ya Mali, ambayo ilitolewa hatua ya 16 bora na Burkina Faso.

## Simba, JKT TZ heshima jeshini

INATOKA UK. 24

Mketo, alisema timu yao imejiandaa vizuri kuwakabili Simba na wamejipanga kuhakikisha wanatumia vizuri uwanja wao wa nyumbani.

Mketo alisema wamefanyia kazi mapungufu waliyokuwa nayo kwa sababu hawakuwa na matokeo mazuri katika mechi zilizopita na wamejiandaa vizuri kufungua uwanja wao kwa kuvuna pointi tatu muhimu dhidi ya Simba.

“Tumefunga mabao chache na kuruhusu bao nyingi, lakini tumerekebisha mapungufu yetu ikiwamo safu ya ulinzi, tunaamini hatuwezi kurudia makosa ya nyuma. Tutacheza kama watakavyokuja wapinzani wetu Simba.

Tutacheza kwa kuwaheshimu na tutachukuwa tahadhari kubwa kulingana na ubora wa kikosi cha Simba kuanzia safu ya ulinzi na washambuliaji kuhakikisha tunafanikiwa kuwazuia,“ alisema Mketo.



Michezo
Alhamisi Februari 15, 2024
Nipashe

Díaz: Bao langu ni maalum kwa Bellingham UKURASA 21





Mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki (kushoto), akiteta jambo na kipa wa timu hiyo, Djigui Diarra baada ya kumaliza mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya KMC itakayochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani, Morogoro keshokutwa. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAVUNJA REKODI LIGI KUU

## Vinara hao wavuna pointi nyingi mzunguko wa kwanza msimu huu...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

BAADA ya kumaliza mechi za mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga imevunja rekodi yake iliyowekwa msimu uliopita kwa kukusanya pointi 40, mbili zaidi ya zile za walizovuna katika msimu wa 2022/2023, imefahamika.

Kwa mujibu wa takwimu za dawati la Nipashe, msimu uliopita, Yanga ilifikisha pointi 38, wakati ilipomaliza mechi zake 15 za mzunguko wa kwanza.

Takwimu zinaonyesha Yanga pia imevunja rekodi ya mabao msimu huu, ikitikisa nyavu mara 36, ikiwa na ongezeko la mabao maneno ya msimu uliopita ambapo mpaka inamaliza mechi za mzunguko wa kwanza ilikuwa imepachika magoli 28.

Kwa upande wa wafungaji, hadi mechi 15 za msimu uliopita, straika wake tegemeo wakati huo, Mkongomani Fiston Mayele alikuwa amepachika mabao 10, ambayo kwa msimu huu mpaka mzunguko wa kwanza unamalizika, idadi hiyo anayo kiungo mshambuliaji, raia wa Burkina Faso, Stephane Aziz Ki.

Yanga haijafunga bao katika mechi moja tu kati ya 15 za mzunguko wa kwanza, ilipotoka suluhu dhidi ya Kagera Sugar, Februari 2, mwaka huu, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba mkoani, Kagera lakini imekuwa imepata angalau bao moja na zaidi katika mechi zote, ikiwamo hata ile iliyopoteza dhidi ya Ihefu.

Takwimu zinaonyesha Yanga imeshinda mechi 13, sare moja na kupoteza moja, ikifunga mabao 36 na kuruhusu wavu wake kuguswa mara nane, kama ilivyokuwa katika mwisho wa mzunguko wa msimu uliopita.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, amesema kitakwimu, Yanga ya msimu huu ni bora zaidi kuliko ya msimu uliopita mpaka kufikia mzunguko wa kwanza unapomalizika.

„Ni kweli kabisa takwimu za msimu huu zinatubeba sana mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, katika pointi 45 ambazo ilipaswa tuchukue mzunguko wa kwanza tumeziacha tano tu, tumechukua 40, ni mafanikio makubwa sana msimu huu kwa sababu msimu uliopita hatukufanya hivi,“ alisema Kamwe.

Pointi tano ambazo Yanga imezikosa ni zile ambazo iliziacha kwa kufungwa

INAENDELEA UK. 23

## Simba, JKT TZ heshima jeshini

**Na Saada Akida**

HESHIMA na nidhamu ndio silaha muhimu ambayo Simba itatumia kuelekea mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya JKT Tanzania itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo ulioko Mbweni, Dar es Salaam.

Wekundu wa Msimbazi watashuka kwa mara ya kwanza kwenye uwanja huo ambao umepata baraka za Bodi ya Ligi hivi karibuni, huku kila timu ikihitaji ushindi kujiimarisha na kuweka rekodi nzuri.

Simba imekuwa na rekodi nzuri dhidi ya Maafande hao, ikipata ushindi wa bao 1-0 hapo Desemba 14, 2021 na Machi 3, mwaka huo huo walifanikiwa kuwafunga JKT Tanzania wakiwa nyumbani mabao 3-0, Oktoba 4, 2020, walishinda 4-0 Simba ikiwa wenyeji na Februari 7, mwaka huo Simba aliibuka na ushindi wa bao 1-0.

Desema 14, 2021, Simba waliibuka na ushindi wa bao 1-0, Agosti 29,2019, walishinda 3-1, Aprili 30, 2019 JKT Tanzania iliibuka na ushindi wa bao 1-0 huku Novemba 3, 2018 Simba iliendeleza ubabe wake kwa kuondoka na ushindi wa mabao 2-0 huku mwaka 2017 wekundu hao waliibuka na ushindi mnono wa magoli 7-0.

Kuelekea mchezo wa leo, Kocha wa Makipa wa Simba, Daniel Cadena, amesema wanaiheshimu JKT Tanzania na wamefanya maandalizi mazuri kwa sababu wanahitaji alama tatu muhimu kutoka katika mchezo huo.

Cadena alisema wanaheshimu timu yoyote wanayocheza nao kwa sababu inashiriki Ligi Kuu, hivyo anaimami wataingia wakiwa na mipango ya kutafuta ushindi ili kujiweka katika msimamo wa ligi.

„Tumefanya maandalizi mazuri, licha ya kutoka safari ndefu na kucheza mechi ngumu, tumerejea nyumbani na tuko tayari kwa ajili ya kuwakabili JKT Tanzania ili kusaka pointi tatu muhimu,“ alisema Cadena.

Nahodha wa Simba, Mohamed Hussein ‚Zimbwe Jr‘ alisema maandalizi ya mechi hiyo yapo vizuri, mchezo hautakuwa rahisi kwa sababu wanapokutana na JKT Tanzania wanapata changamoto kupata ushindi.

“Kama wachezaji tunafuata maelekezo ya benchi na kuhamishia kwenye uwanja wa mechi kutafuta ushindi, bado tupo katika nafasi nzuri na tunahitaji sana alama tatu katika mchezo wetu wa kesho (leo),” alisema beki huyo.

Aliongeza kitendo cha Kocha Mkuu (Abdelhak Benchikha) kutoa nafasi kwa kila mtu ni kuhakikisha wanapambana kusaidia timu kupata matokeo mazuri.

Kocha Msaidizi wa JKT Tanzania, George

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >